


UKURASA 20

Gigy Money aendelea kusota

## Faida kedekede za kitunguu maji kwa afya ya mwanadamu



UKURASA 7

## MAISHA

Mei 9, 2021 Nipashe Baba, Mama na Mwana Jumapili



HARUSI

Ukurasa 12



Ukurasa 15 MAISHA NI NYUMBA

Umuhimu wa malighafi bora katika ujenzi nyumba imara

VIPAPATIO VYA KUOKA

Ukurasa 14




# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Mei 9, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com


ISSN 0856 • No. 0580575




BAKI NA RANGI YAKO

# USHUHUDA MZITO

**MZEE** Mwinyi azindua kitabu, aibua mambo nyeti, Samia akiri ni mafunzo makubwa... *Endelea uk.2*



## Mtoto wa TB Joshua afunga ndoa Tanzania

UKURASA 2

UKURASA WA 3

## SERIKALI YAINGILIA KATI MAITI ILIYOZUIWA KCMC KISA DENI MILIONI 3.5/-

MKUU wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, ametatua mvutano uliodumu kwa siku saba wa kuzuiwa maiti ya Bauda Nkya (68), inayodaiwa kukwama katika Hospitali ya Rufani ya KCMC. Mwili wa Bauda ambaye ni mkazi wa Kitongoji cha Muro, Kijiji cha Nshara, Machame...



Rais Samia Suluhu Hassan na Rais mstaafu wa Awamu ya Pili, Mzee Ali Hassan Mwinyi, wakinyanyua juu kitabu cha historia ya maisha ya Mzee Mwinyi, baada ya kukizindua, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## DONDOO KITABU CHA MWINYI

1. Zanzibar kujiunga na OIC
2. Vuguvugu la kuanzishwa Tanganyika
3. Nyerere kumwita na kumkaripia
4. Kugoma kupanda gari la polisi
5. Kujiuzulu uwaziri
6. Kutukanwa matusi ya nguoni
7. Kuondoka nyumba ya serikali
8. Kuonekana msaliti wa Ujamaa
9. Kurejeshewa mifuko ya saruji
10. Dk. Mengi kupewa ulinzi
11. Kutoalikwa Mei Mosi 1995
12. Mizengwe ndani ya CCM
13. Siri ya kuishi maisha marefu
14. Hajawahi kukopa maishani

## Huu ndio undani kero za mikopo elimu ya juu

UKURASA 4

**MICHEZO** MWAKINYO ATAHADHARISHWA AKIJIANDAA KUMVAA BRENDON UK. 23

MAONI, KATUNI UK.6

# Binti wa TB Joshua aolewa Tanzania

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

IMEISHA hiyo! Ndivyo unavyoweza kusema baada ya mtoto wa Mhubiri wa injili maarufu Afrika, Nabii TB Joshua wa Kanisa la Church of All Nations la Nigeria, Serah Joshua, kufunga pingu za maisha na Brian Moshi, raia wa Tanzania.

Ndoa ya wawili hao, Serah anayeishi Lagos, Nigeria na Moshi, mkazi wa Sinoni jijini Arusha, ilifungwa jana mchana katika Parokia ya Moyo Safi wa Bikira Maria iliyoko Ungalimited Jimbo Kuu Katoliki la Arusha.

Misa maalum ya ndoa hiyo iliongozwa na Paroko wa Kanisa hilo, Padri Festus Mangwangi, na baadaye fungate kufanyika Ukumbi wa Lake Nyasa ulioko AICC, Arusha.

Kabla ya kufungwa kwa ndoa hiyo, Paroko Mangwangwi alisema: "Leo (jana) tumeunganisha Tanzania na Nigeria. Hayo ni malengo ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, kutaka Bara la Afrika liwe kitu kimoja. Sasa yametimia baada ya ndoa hii takatifu.

"Vitu vinavyounganisha watu ni masomo na kuoana. Yanapotokea mambo hayo huondoa uwezekano wa kubagua. Serah huko Nigeria ameona wanaume wengi, lakini umempenda Brian na Brian hapa Sinoni au Marekani, uliona wengi.

"Lakini umemchagua Serah. Wanangu ninawaombea mkazae matunda mema kwa sifa na utukufu wa Mungu Baba," alisema.

Kwa mujibu wa Padri Mangwangi, ndoa hiyo ya mume na mke mmoja kwa taratibu za Kanisa Katoliki, ilitangazwa kanisani huko mara tatu kuanzia April 11 mwaka huu hadi Mei 2 na hakukujitokeza pingamizi, hivyo kanisa likakubali kufungwa kwa ndoa hiyo.

**PAROKO ATAKA WATOTO 8**

Katika ibada hiyo ya ndoa, Padri Mangwangi aliwataka maharusi hao kuzaa watoto wanane ili kanisa lipate watawa watakaosaidia kazi ya kuhuburi neno la Mungu.

Ndoa hiyo ilihudhuriwa na wageni mbalimbali kutoka Jiji la Lagos, Nigeria pamoja na Marekani wanakosoma wanandoa hao.

**NI NDOA YA MSETO**

Baada ya kuwapo minong'ono mingi kuhusu taswira ya ndoa hiyo Kikristo, Padri Mangwangi alisema ndoa ya Brian na Serah ni ya 'mseto.'

Alisema ndoa ya mseto inaruhusu kila mmoja kubaki kwenye imani yake, isipokuwa watoto watakaozaliwa wanakuwa wakatoliki.

Brian Moshi (Mtanzania) ni muumini wa Kanisa Katoliki na Serah Joshua ni Mpentekoste. Awali, maharusi hao walishafunga ndoa ya kwanza ya kiserikali Nigeria na ya Kipentekoste Dubai huko Falme za Kiarabu.

**MKE WA TB JOSHUA**

Akiwa jijini Arusha, mke wa Nabii TB Joshua, Evelyn Joshua, kwa furaha alisema amefika Tanzania kwa mara ya kwanza kushuhudia ndoa ya binti yake.

"Sasa nimefungua milango ya kuja Tanzania kila mara na ndugu zangu Watanzania hasa wakwe zetu kuja Nigeria kwa kuwa ni nyumbani, na hii ni baada ya muunganiko wa ndoa ya vijana hawa wawili.

"Mume wangu (TB Joshua) anawasalimu na amenituma nilete salamu nyingi kwa Watanzania. Nimefurahi kwa upendo huu nina cha kusimulia nikirudi Nigeria," alisema.



Maharusi watarajiwa Binti wa Nabii TB Joshua wa Lagos nchini Nigeria, Serah Joshua na Brian Moshi wa Sinoni Arusha, wakitoka kwenye nyumba ya mapadre wa Parokia ya Moyo Safi wa Bikira Maria Ungalimited, wakijiandaa kuingia kanisani kufunga ndoa, jijini Arusha jana. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Ushuhuda mzito kitabu cha Mwinyi

**Na Romana Mallya**

ILIKUWA siku ya Ijumaa Mei 8, mwaka 1925, alipozaliwa mtoto wa kiume pekee kati ya watoto watano wa Mzee Hassan Mwinyi Magondi na Asha Mwinyi Shehe katika Kijiji cha Kivule wilayani Mkuranga mkoani Pwani.

Ndivyo Profesa Rwekaza Mukandala kutoka Kigoda cha Mwalimu Nyerere Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alivyoanza kuwasilisha uchambuzi wa kitabu cha Rais wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi, kijulikanacho kama 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu'.

Katika kitabu hicho cha kurasa 491 zilizogawanywa kwenye sura 31, viambatanisho na picha nyingi, ambacho utangulizi wake umeandikwa na Hayati Rais Benjamin Mkapa, Mwinyi anaanika ushuhuda wa mambo mazito ya uongozi wake ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na serikalini, akitumia maneno 139,307.

Mbele ya Mgeni Rasmi, Rais Samia Suluhu Hassan, Profesa Mkandala wakati wa uzinduzi wa kitabu hicho jijini Dar es Salaam jana, alisema Mwinyi ametoa majibu ya baadhi ya maswali mengi ambayo yamekuwa yakimfuata kila alipokwenda.

Alitaja baadhi ya maswali hayo kuwa ni: Asili yake ni Tanzania Bara au Tanzania Zanzibar? Kwa nini aliachia ngazi uwaziri mwaka 1977? Ilikuwa hiari? au alishinikizwa na Mwalimu? Ilikuwaje akamrithi Alhaji Aboud Jumbe mwaka 1984 wakati kulikuwa na Wazanzibar wengine mashuhuri zaidi na walioutaka huo urais? Ilikuaje akamridhi Mwalimu hata kama hakuwa chaguo lake la kwanza?

Profesa Mukandala anataja anachokiona kuwa ni siri ya Mwinyi kuishi maisha marefu, akikinukuu katika kitabu hicho kuwa "Mzee Rukhsa hajawahi kukopa katika maisha yake".

Vilevile, mmoja wa watoto wa Mwinyi alibainisha jana alasiri kuwa baba yao huyo hajawahi kunywa pombe.

Katika kitabu hicho, Mwinyi pia anabainisha safari yake ya utumishi wa umma na namna alivyokumbana na ubaguzi wa rangi wakati wa harakati zake za kupata elimu, huku nyumbani nako akitakiwa kuhakikisha anakusanya vyombo asubuhi na kuviosha kabla ya kwenda shuleni.

Katika kitabu hicho, Mwinyi anakumbusha alipokataa kupanda gari la polisi alipoitwa Ikulu, kipindi hicho akiwa Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Chama Muhimu cha Walima Karafuu kilipotaifishwa mwaka 1970.

"Siku moja alipata simu kwamba anaitwa Ikulu Zanzibar na gari la polisi likamfuata ila akakataa kulipanda, akisema kwa kuwa siyo mfungwa wala mtuhumiwa, atakwenda mwenyewe.

"Walifukuzana na polisi hadi Ikulu huku gari la polisi likiwasha taa na king'ora, hatimaye alikwenda kumsalimu Rais Abeid Karume, akamwambia 'Rais Nyerere ameomba majina mawili ili amteue mmoja awe waziri na kuelezwa kuwa jina lake ni mojawapo na alishauriwa asikilize taarifa ya habari saa mbili usiku'," Prof. Mukandala alisema na kumkuu Mwinyi akibainisha:

"Moyo wangu ulijaa mchanganyiko wa uoga na furaha isiyoelekeza, tamaa ya kupata na hofu ya kukosa". Usiku ule Mwinyi aliteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na katika kitabu hicho ananukuliwa akisema "nililala mwalimu nikaamka waziri katika Serikali ya Muungano'. Akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, mwaka 1977 Mwinyi ilibidi ajiuzulu baada ya mauaji huko Mwanza na Shinyanga. Katika kitabu chake, Mwinyi alifanya hivyo bila shinikizo kutoka kwa Mwalimu Nyerere.

Ananukuu sehemu ya barua aliyoiandika kwa Rais Nyerere ambayo imeambatanishwa kwenye kitabu hicho ikisema "Kwa fedheha hii, ninaomba unikubalie nijiuzulu Mwalimu."

Baada ya uteuzi kadhaa, aliteuliwa tena kuwa Waziri Ofisi ya Rais (Muungano) wakati huo akiwa anaishi nyumba ya serikali huku akijenga nyumba yake Oysterbay na akiwa na vifaa vya ujenzi ndani ya nyumba hiyo ya serikali, waziri mwingine akatakiwa kuishi kwenye nyumba hiyo ambaye alimtaka ampishe na aondoke mara moja.

Mwinyi anasema alilazimika kumpisha waziri huyo na vifaa vya ujenzi alimwachia na alipokuwa Rais, "huyo bwana alikuwa na wasiwasi lakini aliendelea kumpa uwaziri".

Katika kitabu hicho, Mwinyi anabainisha sababu za serikali kuamua kumpa ulinzi Dk. Reginald Mengi, sakata la Zanzibar kujiunga Jumuiya ya Nchi za Kiislamu (OIC), vuguvugu la kuanzishwa kwa Serikali ya Tanganyika, Mwalimu Nyerere kumwita na kumkaripia na kutukanwa matusi.

Mengine yaliyomo ndani ya kitabu hicho ni Mwinyi kuitwa msaliti wa Ujamaa, kutoalikwa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani mwaka 1995 na mizengwe ndani ya CCM.

SAMIA: MAFUNZO MAKUBWA

Rais Samia alisema amekisoma mara mbili kitabu hicho na kubainisha kimesheheni mambo mengi yenye mafunzo makubwa, kikizinduliwa siku ambayo Mwinyi alikuwa anaadhimisha umri wa miaka 96.

Alisema kitabu hicho siyo tu kitasaidia Watanzania kumfahamu, bali pia kina maelezo ya historia ya taifa.

"Ninakupongeza kwa kuandika kitabu chako kwa lugha ya Kiswahili, lugha ambayo umeibobea na inayoeleweka na kutumiwa na Watanzania wengi, nimekisoma kitabu chako mara mbili," alisema.

Rais Samia alisema alivyosoma mara ya kwanza, aliyoyakuta ndani yalimfanya ashtuke na kusema 'mtu wa maarifa na hekima zote kama Mwinyi yamempata yote haya, mimi je?'.

"Kikanipa woga kidogo, lakini kutokana na ufasaha na ladha ya lugha na maneno yaliyotumika ndani, nikakirudia tena kukisoma, niliposoma mara ya pili uoga ukanitoka, nikasema kazi iendelee," alisema.

Alisema ameona kuna mambo yanayomfanya Mzee Mwinyi awe alivyo ikiwa ni pamoja na ucha Mungu huku akimpongeza kwa kusimamia mageuzi ya kisiasa nchini.

Rais Samia alisema Mwinyi ni baba wa mageuzi nchini ambaye alisimamia mageuzi ya kiuchumi kwa kuwa wakati anaingia madarakani, hali ilikuwa mbaya ukiwamo upandaji wa bei ya mafuta, ukame, kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, vita vya Kagera na masharti magumu yaliyotolewa na wafadhili kipindi hicho.

"Kitabu kinatufundisha mambo mengi hususani viongozi, anatufundisha uongozi wa nchi hautafutwi bali unatoka kwa Mungu," alisema Rais Samia huku akisisitiza viongozi kutolipa kisasi kama alivyofanya Mwinyi kwa waziri aliyemtimua kwenye nyumba ya serikali.

HABARI KITAIFA

# LATRA yasikia kilio wenye ulemavu

Na Romana Mallya

BARAZA la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA), baada ya kupokea kero wanazozipata watu wenye ulemavu wasioona kuhusu ulanguzi wa tiketi na kunyanyaswa kwenye mabasi, limezindua kitabu maalum cha lugha ya nukta nundu ili kuwawezesha kukata tiketi kieletroniki kupitia simu zao za kiganjani.

Kitabu hicho ambacho kitagawiwa bure kwa kundi hilo nchini, kilizinduliwa juzi mkoani Dar es Salaam na Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kisare Makori, baada ya kuandaliwa na LATRA.

Katika taarifa yake iliyosomwa kwa niaba yake na Ofisa Tarafa Kibamba, Beatrice Mbawala, alisema mfumo huo unaepusha upandishaji nauli kiholela, kuondoa kero vituoni na kwa upande wa wamiliki wa mabasi kuweza kukopesheka kirahisi na serikali kupata takwimu sahihi.

Aliwataka wamiliki wa mabasi pamoja na Kituo cha Mabasi cha Magufuli kutumia mfumo wa utoaji wa tiketi kwa njia ya kieletroniki.

"Mafunzo haya ni muhimu kwa kundi hili ili liweze kutumia mfumo huu wa kieletroniki, nina imani hatutegemei kama serikali, kundi hili kupata tabu tena ikiwamo kutapeliwa," alisema.

Mwenyekiti wa LATRA, Dk. George Makuke, alisema wameamua kufanya mafunzo kwa kundi hilo na kutoa kitabu hicho ili kiwawezeshe hatua za ukataji wa tiketi kwa kimtandao ili wasibaki nyuma katika teknolojia ambayo kila siku imekuwa ikikua kwa kasi.

Alisema wameanza na mafunzo kwa kundi hilo kwa Mkoa wa Dar es Salaam na wanatarajia yafanyike mikoa mbalimbali ili kuwafikia huko walipo.

"Vitabu hivi tutapeleka mikoani kwenye ofisi zetu ili visambazwe kwa watu wenye kundi hili na vitatolewa bure kwao kwa sababu baraza linagharamia, leo tunatoa mafunzo kwao kwa watu zaidi ya 40 ambao wamepatikana kupitia vyama vyao," alisema.

Kaimu Katibu Mtendaji wa LATRA, Leo Ngowi, alisema baraza lina wajibu wa kusikiliza makundi yote na kupokea maoni yao na kuyawasilisha serikalini ili kupatiwa ufumbuzi.

"Serikali imejitahidi kuhakikisha kwamba kuna mfumo wa kukatisha tiketi kwa njia ya kieletroniki, kundi hili lilikuwa halijapewa mafunzo ya namna ya kutumia hiki kifaa, kupitia kitabu hiki tunachokizindua leo ambacho kimetumia nukta nundu watafahamu namna ya kukata tiketi kimtandao," alisema.

Alisema baada ya mafunzo hayo itakuwa ni haki yao kudai tiketi za kieletroniki pindi wapandapo kwenye vyombo vya usafiri.

Alisema kundi hilo limekuwa likinyanyasika kwa muda mrefu kwa kupandishiwa nauli na majina yao yamekuwa hayaandikwi vizuri kwenye tiketi na taarifa zao hazipatikani.

"Mfumo huu wa kieletroniki tunaamini utatatua matatizo haya yote na kutozwa nauli halali, mafunzo haya yatafanyika pia jijini Dodoma ndani ya mwezi huu. Elimu hii itatolewa pia kwa wanafunzi wa vyuo na baada ya mafunzo hayo abiria wataanza kupanda mabasi kwa kupanga foleni na tutaanza na mabasi ya mjini lengo ni kuleta mapinduzi kwenye sekta ya usafiri.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo kwa Wasioona Tanzania, Kiongo Itambo, alisema moja ya matatizo wanayokutana nayo vituo vya mabasi ni kutozwa nauli kubwa ambayo haiendani na ubora wa basi lenyewe na hiyo inatokana na wao kutoona.

Alisema anaamini matumizi ya kieletroniki yataondoa kero hiyo ambayo kwao ilikuwa kubwa na wakati mwingine walishindwa kuwatambua waliowakatia tiketi ili wapate haki zao.

# Serikali yaingilia kati maiti iliyozuiwa KCMC deni mil. 3/-

Na Godfrey Mushi, HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, ametatua mvutano uliodumu kwa siku saba wa kuzuiwa maiti ya Bauda Nkya (68), inayodaiwa kukwama katika Hospitali ya Rufani ya KCMC.

Mwili wa Bauda ambaye ni mkazi wa Kitongoji cha Muro, Kijiji cha Nshara, Machame Kaskazini, unadaiwa kuzuiwa kuchukuliwa kwa ajili ya maziko baada ya kushindwa kulipa gharama ya zaidi ya Sh. 3.5.

Jana, alipokwenda katika Kijiji cha Nshara kuwapa pole wafiwa ambao ni kaya inayohudumiwa kupitia ruzuku ya uhaulishaji wa kaya maskini inayotekelezwa na Mfuko Maendeleo ya Jamii (TASAF), Ole Sabaya, alisema serikali imeliona jambo hilo na imeamua kubeba mzigo huo wa gharama.

"Nimekuja kuwapa pole kwa msiba huu. Serikali imekisikia kilio chenu na kuiona huzuni yenu na uchumi mlio nao. Niahidi hapa kwamba tutalisimamia jambo hili msihuzunike.

"Ofisi yangu kupitia DAS (Katibu Tawala wa Wilaya), Upendo Wella, utabeba jukumu hilo la malipo kutokana na uduni wa familia hii.

"Kimsingi, hii familia ni duni na ukitazama kabisa haina uwezo wa kulipa Sh. milioni 3.5, hiyo ni kama miujiza kwao.

"Kwa hiyo anzeni maandalizi ya kuzika, ofisi yangu kupitia kwa DAS, itafanya mawasiliano na huu mwili utaletwa kesho hapa (leo) nyumbani kuzikwa," alisema. Bibi huyo alifariki dunia Mei 2 mwaka huu, chanzo cha kifo chake kikidaiwa kujikwaa kwenye kisiki na kupata jeraha sehemu ya mguu wake, lililosababisha mguu kuoza.

Akizungumzia kifo cha mama yake, mtoto wa marehemu, Muzaimata Urassa, alisema baada ya mama yao kufariki dunia katika Hospitali ya Rufani ya KCMC, walipewa taarifa ya gharama hiyo ya Sh. milioni 3.5.

Alisema kwa siku kadhaa wamekuwa wakiomba kuchukua mwili wa mama yao baada ya kupunguza gharama hiyo kwa kupeleka kiasi Sh. milioni 1.1 lakini hawakukubaliwa kuuchukua.

Hata hivyo, alipoulizwa kuhusu malalamiko hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya KCMC, Profesa Gileard Masenga, alisema hana taarifa hiyo. "Kama yupo mtu ameshindwa kulipa gharama za matibabu, kuna utaratibu ambao unafanyika ikiwamo kusamehewa," Profesa Masenga alisema.



Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, akiwa ameshika mkate uliotengenezwa kwa unga wa muhogo, alipotembelea mabanda ya wajasiriamali katika maonyesho ya wadau wa zao la muhogo, jijini Dodoma juzi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Mbunge Morogoro atuliza mgomo madereva

Na Ashton Balaigwa, MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, AbdulAziz Abood, amewatuliza na kuwataka kusitisha mgomo madereva wa pikipiki za miguu mitatu, maarufu bajaj, katika Manispaa ya Morogoro ili kuziwakilisha kero zao kwa wahusika.

Abood aliyelazimika kuondoka bungeni linakoendelea Bunge la Bajeti na kurejea jimboni kwa ajili ya mazungumzo na madereva hao, alisema pamoja na kuwapo kero hizo kwa muda mrefu bila kupatiwa ufumbuzi, wanapaswa kusitisha mgomo huo.

Akiwakilisha kero zilizosabisha mgomo huo, katika kikao cha pamoja na mbunge huyo, Katibu wa Umoja wa Waendesha Bajaj Morogoro (UWABAMO), Omary Masoud, alisema kero kuu ni kuzuiwa kuingia katika maeneo ya mjini na katazo la kutumia baadhi ya njia kwa kigezo cha kuleta foleni pindi wanaposafirisha abiria.

Alisema kero zingine ni Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kufuta vituo vya kutolea huduma katika maeneo ya mjini ambako wanapaswa kushusha abiria na kupakia pamoja na ukamataji bila sababu unaofanywa na maofisa wa TARURA na LATRA kunakoambatana na kuwatoza faini kubwa za kati ya Sh. 200,000 na 300,000.

Alibainisha kuwa alisema mapendekezo yao ni pamoja na bajaj zote zinazosafirisha abiria kutoka Bigwa, Kichangani na Kilakala zishushe eneo la Mwere na zile zinatoka Kasanga, Chamwino na SUA zitumie njia ya Konga na ziishie eneo la Chipukizi ili kupunguza msongamano katikati ya mji.

Katibu huyo alisema kwa kufanya hivyo, manispaa itakusanya mapato yake ya zaidi ya Sh. milioni 1.4 kwa siku ambayo yamekuwa yakipotea kutokana na madereva kukimbia kukwepa ushuru kutokana na kutotengewa maeneo rafiki ya kufanya kazi, hasa mjini.

Akijibu hoja hizo, Abood alisema serikali iliyopo madarakani haina chuki na vijana hao wanaofanya biashara katika Manispaa hiyo ya Morogoro, bali wanapaswa kufuata taratibu zilizowekwa.

Mbunge huyo aliahidi kutatua kero hizo kwa kuzifikisha kwa Meya wa Manispaa hiyo, Paschal Kianga, ili zipatiwe ufumbuzi huku akiwasisitiza kusitisha mgomo huo.

Awali, katika kikao cha pamoja na madereva wa bajaji hao, Manispaa ya Morogoro kupitia kwa Mkurugenzi wake, Sheila Lukuba, ilitoa mapendekezo kuwa bajaj zote zinazotoka njia ya Kihonda, haziruhusiwi kuvuka taa za Msamvu na zikifika huko, zitumie barabara ya Mei Mosi kwenda Kikundi au Mwembesongo hadi Hospitali ya Mkoa.

Mkurugenzi huyo alielekeza bajaj zinazotoka SUA, Mindu, Kasanga, Chamwino na Idiva/Kihonda Maghorofani, zitaishia eneo la Kikundi wakati zile zinazotoka barabara ya Boma zitapitia Nguzo na kuishia Hospitali ya Mkoa, agizo ambalo lilipingwa na waendesha bajaj hao.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA FOMU MADAI .3**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya NGORONGORO**
**Kituo Cha LOLIONDO Mkoa ARUSHA**
**Shauri la madai/Ndoa Na……..08/2021**
**Jina la Mdai RAPHAEL JOHN SIUMBU**
**Jina la Mdaiwa SPENDINA SELHAJI NGIMBA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo )**

Kwa **SPENDINA SELHAJI NGIMBA**
Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta /Wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai) 1 OMBI LA MTALAKA

**2. MATUNZO YA WATOTO**
**3. GHARAMA ZA KESI**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 17 Mwezi 05 Mwaka 2021 saa 08:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautahudhuria siku iliyiotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo .

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 04 Mwezi 05 Mwaka 2021.

……………………………………
**HAKIMU**

MAKALA MAALUM

# Undani kero mikopo elimu ya juu

## ●Samia aingilia kutatua, CAG Spika Ndugai wahadharisha

Na Sanula Athanas

UNAPOZUNGUMZIA Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) siyo msamiati mgeni kwa Watanzania na hata kimataifa.

Taasisi hiyo yenye umri wa miaka 17, hivi sasa imegeuka kuwa mjadala mkubwa uliochukua sura ya kitaifa ukiangazia mtazamo wa mapitio ya baadhi ya majukumu yake, malalamiko ya namna inavyotoa huduma na kufumuliwa kwa sura na uwajibikaji wake.

Wakati kuna mtazamo huo, ni siku chache zilizopita, mamlaka ya juu kitaifa, chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, ilifanya mapitio yenye maslahi chanya kisiasa na kiuchumi kwa walengwa wake.

Je, HESLB ni nini? Ni taasisi iliyoanzishwa kisheria mwaka 2004 kuwahudumia walengwa wa mikopo na ruzuku ya elimu ya juu nchini, huku ikiwajibika kwa ukusanyaji wa madeni ya mikopo na kuwa kiunganishi na mratibu wa shughuli zote za upatikanaji wa fedha zinazotumika kuwezesha mikopo hiyo.

Licha ya bodi hiyo kuanzishwa mwaka 2004, utoaji wa mikopo hiyo nchini ulianza mwaka 1994, yaani miaka 27 iliyopita, walengwa wakuu ni wenye uwezo duni kiuchumi.

### KIINI CHA MJADALA

Ukirejewa mfumo wa mikopo ya elimu ya juu, ilianza kwa wanafunzi wa baadhi ya vyuo waliopatiwa mikopo kugharamia sehemu ya ada ya masomo na mahitaji mengine, sehemu iliyobaki serikali ilichangia.

Hata hivyo, utoaji wa mikopo hiyo uliendelea kufanyiwa marekebisho yanayombebesha zaidi gharama mwanafunzi, ingawa inaelezwa mifumo ya marejesho hayo yasiyo na riba mwanzoni, haikuwa bayana.

Kwa maana hiyo, HESLB ilizaliwa kama mkono rasmi wa serikali kuwajibikia jukumu hilo, nyuma yake ikisimamiwa na nguvu ya kisheria mahususi kwa jukumu hilo.

Ukaguzi Maalum wa Hesabu za HESLB uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ambao ripoti yake iliwasilishwa kwa Rais Machi mwaka huu, umeorodhesha mlolongo wa dosari katika usimamizi na mfumo wa ukusanyaji madeni.

CAG Charles Kichere anasema HESLB inaelemewa na kasoro za: Ucheleweshaji katika kutoa mikopo; ulipaji na urejeshaji hafifu; na baadhi ya mikopo kutolipwa.

Vilevile, CAG anadokeza bodi hiyo imeendelea kuitegemea serikali kwa wastani wa theluthi mbili ya bajeti yake (asilimia 66), huku upande wa pili utendaji wa ndani nao hauridhishi, hususani katika jukumu muhimu la ufuatiliaji mikopo.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, mwenendo wa sasa wa HESLB unatia shaka uhai wake, vivyo hivyo kwa hatima ya wanufaika wapya, katika mtazamo mpana wa kitaifa kuwa mpango endelevu.

CAG anatoa ushuhuda wa udhaifu katika ukusanyaji mikopo, kwamba ndani ya mwaka mmoja, kati ya mwaka wa fedha 2015/16 na 2016/17 tayari kulikuwa na ongezeko la wadaiwa sugu 128,278.

"Hata hivyo, taarifa zilizotolewa na bodi, zilionesha kulikuwa na wadaiwa sugu wa mikopo wapatao 18 pekee.

"Kwa mujibu wa kumbukumbu za bodi, ni wadaiwa sugu wawili tu waliokiuka masharti ya ulipaji wa mikopo waliofikishwa mahakamani," CAG anabainisha.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anasema ukaguzi wake ulibaini katika mwaka wa fedha 2015/16, waliokaidi kulipa mikopo walikuwa 163,394 na kwa mwaka uliofuata walikuwa 291,672. Kwa maana hiyo, ongezeko la wadaiwa sugu ni 128,278 iliyokwishatajwa.

"Ilibainika wakati wa ukaguzi kuwa bodi ilikusanya Sh. bilioni 221 tu kati ya Sh. trilioni 2.4 kutoka kwa wadaiwa waliopatikana kwa miaka mitano ya fedha kuanzia mwaka 2012/13 hadi 2016/17.

"Upatikanaji endelevu wa rasilimali kwa wanufaika wapya wa mikopo uko hatarini kwani bodi haitakuwa na fedha za kutosha kuwakopesha wanafunzi wapya wanaostahili.

"Utegemezi wa bajeti ya nyongeza kutoka serikali kuu kwa utendaji na shughuli endelevu za bodi utaendelea," CAG anatahadharisha.

### KILIO CHA MAKATO

Jicho la CAG katika Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, linaibua tena alichokiita 'uonevu katika makato' yanayohusu HESLB.

CAG Kichere ananyoshea kidole kuwapo ukiukwaji wa makato katika malipo ya mishahara ya watumishi wa mamlaka hizo za kiserikali, ikielekezwa kisheria ni sharti mtumishi alipwe mshahara usiopungua theluthi moja ya ujira halisi.

Anarejea kifungu cha tatu cha Sheria ya Maofisa Waliobainishwa (Urejeshwaji wa Madeni) Sheria Na. 7 ya Mwaka 1970 na Mwongozo wenye Kumbukumbu Namba 26/46/01/1/66 wa Novemba 28, 2012, unaoweka masharti watumishi wanapaswa kulipwa si chini ya theluthi moja ya mishahara yao ya kila mwezi.

CAG anabainisha kuwa ukaguzi wake umebaini makato ya HESLB yamechangia kuwapo tatizo hilo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

"Uchambuzi uliofanywa katika mamlaka 35, ulibaini watumishi 3,038 waliokuwa wakipokea chini ya theluthi moja ya mishahara yao," CAG Kichere anasema.

CAG anabainisha kasoro hujitokeza pale mdaiwa wa bodi anaruhusiwa kuchukua mikopo mingine yenye makato yanayomfanya kukiuka alipwe chini ya theluthi moja ya mshahara, huku katika baadhi ya halmashauri kukibainika kuwapo watumishi wasiolipwa kitu kutokana na mikopo inayowakabili.

"Nilibaini kuwa hali hii ilichangiwa na ulipaji wa deni la HESLB ambalo hutozwa asilimia 15 ya mshahara wa mtumishi ambaye ni mnufaika wa mkopo," CAG anasema.

Anataja baadhi ya halmashauri na idadi ya waathirika wake katika mabano ni: Jiji la Arusha (1); Wilaya za Kiteto (1); Mji Njombe (1); Manispaa ya Temeke (1), Wilaya ya Rombo (3) na Wilaya ya Same (1).

"Ninapata wasiwasi na ustawi wa watumishi hawa katika kupata mahitaji yao muhimu kama vile chakula, mavazi na malazi.

"Hali hii inasababisha watumishi kutumia muda wa kazi kwa shughuli zao binafsi ili kujipatia kipato cha ziada, hali inayoweza kudumaza utoaji wa huduma kwa jamii," CAG anabainisha.

### KUTOKA BUNGENI

Kilio cha mustakabali wa mikopo na uhai wa HESLB pia ni mada inayolikamata Bunge. Spika Job Ndugai analia na malalamiko na kasoro kuhusu bodi hiyo, kwamba hatima yake iko shakani na haibebi sura ya mtoto wa maskini.

Spika Ndugai anazimulika kero za mikopo hiyo kuwa na 'riba' iliyobatizwa jina la tozo ya kutunza thamani ya mkopo (ongezeko la asilimia sita ya mkopo kila mwaka) kwamba ni mzigo kwa mtoto wa maskini.

"Hii ni kweli, maana kumpa mtoto wa maskini mkopo wa elimu halafu unakuja kumdai mkopo na riba siyo sawa, hiyo ni sawa na bi-

INAENDELEA UK. 5



Rais Samia Suluhu Hassan, akiagana na viongozi mbalimbali wa serikali na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), baada ya kulihutubia Taifa katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), mwaka huu kwenye Uwanja wa Kirumba jijini Mwanza. Siku hiyo, Rais alitangaza kufuta utaratibu wa deni la HESLB kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka. **PICHA: MAKTABA**



Mbunge wa Viti Maalum, Esther Matiko



Spika Job Ndugai

# Undani kero mikopo elimu ya juu

INATOKA UK. 4

ashara," anasema.

Spika Ndugai anasema utaratibu huo hauendani na kauli ya kuwasaidia wanafunzi na kwamba utaratibu huo hauna tofauti na wanaokopa fedha za kununua magari.

Mbunge wa Viti Maalum, Esther Matiko (CHADEMA), anapiga hatua zaidi akidai atawasilisha muswada binafsi bungeni wa kurekebisha sheria iliyoanzisha HESLB, kwamba haridhishwi hata kidogo na kinachofanyika.

Huku akitafsiri kinachofanywa na bodi hiyo sasa kwamba ni 'uonevu', Matiko anafafanua: "Serikali ifanye marejeo ya sheria hii ya mikopo ya elimu ya juu.

"Makato ya asilimia 15 ya mshahara wa mwajiriwa ni makubwa mno ukizingatia huyu mtu anakatwa makato mengine ikiwamo PAYE (kodi ya mshahara), bima ya afya na makato mengineyo.

"Hata hiyo penalti ya asilimia 10 kama akishindwa kuanza kulipa mkopo baada ya miaka miwili ni tatizo. Ni sheria kandamizi.

"Huu ni mkopo kwa ajili ya kusaidia watoto wa maskini na yatima. Siyo sawa na mikopo ya benki. Ni kumdidimiza zaidi mtoto wa maskini badala ya kumsaidia."

**RAIS AINGILIA KATI**

Katika hotuba yake ya kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), mwaka huu, Rais Samia alitangaza kufuta utaratibu wa deni kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka, ambayo ni sehemu ya kilio alichowasilisha Mbunge Matiko.

Hata hivyo, mwongozo wa deni husika unabainisha kuwapo makato asilimia moja ya mkopo anaodaiwa mnufaika, ili kuhudumia uendeshaji wa bodi.

Pia kutaendelea kuwapo makato ya asilimia 15 kwenye malipo ya mshahara wa mnufaika kufidia mkopo wake.

Kwa mujibu wa HESLB, mnufaika hupewa kipindi cha miaka miwili kuanza kulipa baada ya kuhitimu masomo, vinginevyo anakumbana na adhabu ya nyongeza ya asilimia 10 ya mkopo wake, adhabu inayozalisha kero nyingine inayolalamikiwa na wadau.

**UAMUZI WA WIZARA**

Jumanne ya wiki hii, ikiwa ni siku tatu baada ya Rais Samia kutangaza kufuta tozo ya asilimia sita, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, alitangaza kufuta tozo ya adhabu ya asilimia 10 kwa wanufaika wanaochelewa kulipa mikopo hiyo.

Profesa Ndalichako aliliarifu Bunge kuwa utekelezaji wa kufutwa kwa tozo hiyo utaanzia Julai Mosi mwaka huu, yaani siku ya kwanza ya mwaka ujao wa fedha.

Waziri huyo pia alitumia fursa hiyo kubainisha mikakati ya serikali kufanyia kazi mapendekezo ya CAG kuinusuru bodi hiyo na hatima ya wanafunzi wakopaji kuwa ni pamoja na kuimarisha mifumo ya kiteknolojia ili kuwa na mifumo rafiki itakayowezesha ukusanyaji wa Sh. bilioni 200 kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema serikali pia itaanzisha kituo mahsusi cha wateja jijini Dar es Salaam ili kuboresha huduma za HESLB kwa wateja hususani katika urejeshaji wa mikopo.

Alibainisha kuwa kwa mwaka ujao wa fedha, serikali kupitia HESLB itasimamia uombaji, uchambuzi na utoaji wa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 500 kwa wanafunzi wahitaji wapatao 148,581.

Kati yao, wanafunzi 50,250 watakuwa wa mwaka wa kwanza na wanaoendelea na masomo 98,331.

**'RIBA' INAVYOUMIZA**

Miaka miwili iliyopita, Nipashe ilizungumza na Meneja wa Habari, Elimu na Mawasiliano wa HESLB, Omega Ngole, aliyetoa takwimu ambazo zilibainisha utaratibu wa deni kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka umesababisha wanufaika wengi kushindwa kumaliza kulipa madeni yao.

Ngole alibainisha kuwa hadi siku ya mazungumzo na Nipashe Agosti 6, 2019), ni wanufaika 11,214 waliofanikiwa kumaliza kulipa madeni yao.

Idadi hiyo ni sawa na asilimia 2.3 ya wanufaika wote 479,779 waliopewa mikopo yenye jumla ya Sh. trilioni 3.889 tangu serikali ilipoanza kuitoa mwaka 1994 hadi siku hiyo ya mazungumzo ya Nipashe na meneja huyo.

Ngole alisema kuwa tangu HESLB ipewe jukumu la kusimamia urejeshwaji wa mikopo hiyo mwaka 2007, wahitimu 11,214 waliofanikwa kumaliza madeni yao, wamelipa jumla ya Sh. bilioni 67.6 na kupewa vyeti.

Meneja huyo alibainisha kuwa jumla ya wahitimu 145,656 walikuwa hawajaanza kulipa mikopo yao ya jumla ya Sh. bilioni 432.5 na wana zaidi ya miaka 10 tangu wahitimu masomo yao.

Kiasi hicho cha fedha kilichokuwa kwa wadaiwa sugu, ni zaidi ya mikopo iliyotolewa na HESLB kwa mwaka wa fedha 2018/19 ambayo ilikuwa Sh. bilioni 427 kwa wanafunzi 123,285.

**NINI KIFANYIKE?**

Aliyekuwa CAG kwa miaka minane kuanzia mwaka 2006, Ludovick Utouh, anaona haja ya mjadala wa kisheria kuhusu urejeshaji wa mikopo hiyo.

Katika mahojiano maalum na Nipashe jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, Utouh alisema: "Mkopo ni pesa ambayo unaipokea ili baadaye uilipe.

"Tulisema tunakopesha watu wasome, waajiriwe na kupitia mshahara wao wa kuajiriwa warudishe deni. Sasa tunasomesha watu wanahitimu lakini hawana ajira.

"Ndiyo maana CAG anasema kuna wadaiwa sugu 128,000 wameongezeka ndani ya mwaka mmoja na watu hao wakati mwingine hata kuwapata katika mifumo maalum inakuwa ni shida.

"Kwa hiyo, mimi ninafikiri tunatakiwa kurudia kufikiria yale mawazo ya kukopesha mtu asome, ahitimu, ajiriwe na kupitia mshahara alipe deni.

"Sasa, kwenye hali yetu hii ambayo hakuna ajira, tutawezaje kurudisha gharama hizo? Tufike mahali tufikirie tena hii mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

"Watu wanasoma kupitia mikopo lakini hawajaajiriwa, ni vipi watarudisha? Kuwe na sheria ya kusema kuwa huyo mtu akimaliza masomo yake bila kupata ajira kwa kipindi fulani nini kifanyike, kuliko kuripoti kwenye vitabu kusema bodi ya mikopo inadai kiasi kikubwa wakati tunajua uwezekano wa kurudisha ni sifuri," anashauri.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako



Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Abdul-Razaq Badru

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Hatua stahiki zichukuliwe kwa viongozi wa mashirika waliokaidi ukaguzi wa CAG

**KATIKA** moja ya habari kubwa katika toleo la jana la Nipashe ni Spika wa Bunge la Tanzania, Job Ndugai, kuibua sakata la mashirika manane ya umma kushindwa kuwasilisha taarifa za fedha kwenye ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Mashirika hayo ni Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Soko la Bidhaa Tanzania (TMX), Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja (UTT), Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), Shirika la Posta Tanzania na Shirika la Reli Tanzania (TRC).

Hatua hiyo imemfanya Spika Ndugai kuiagiza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kuziita bodi za wakurugenzi na menejimenti za mashirika hayo kutoa sababu za kushindwa kufanya hivyo.

Pamoja na kuitwa kujieleza mbele ya PAC, Ndugai alisema mashirika hayo hayajafanyiwa ukaguzi kwa kigezo cha kutokuwa na taarifa na kutoa onyo kwa mengine yenye tabia kama hizo.

Hata hivyo, alisema kutokufanya hivyo ni uzembe wa hali ya juu kwa shirika kukosa hesabu zinazokagulika na kusisitiza kuwa kitendo hicho si cha kuvumiliwa hata kwa chembe yoyote, hivyo viongozi wake waitwe na kuhojiwa ili kutoa sababu zilizowafanya hivyo na hatimaye hatua kuchukuliwa.

Taarifa hiyo ya spika wa Bunge kuhusu mashirika hayo imeonyesha ukiukwaji wa sheria za nchi hasa matakwa ya kila taasisi iliyo chini ya serikali kuwasilisha taarifa zake kwa ajili ya kukaguliwa na CAG. Sababu iliyotolewa na viongozi wa mashirika hayo hazina mashiko bali ni jeuri na kiburi kutoka kwa viongozi wa taasisi hizo.

Lakini jambo kubwa la kujiuliza ni nani aliyewapa kiburi mpaka kushindwa kuwasilisha taarifa kwa ajili ya ukaguzi? Nini kilichojificha nyuma ya pazia ndani ya mashirika hayo?

Miongoni mwa taasisi hizo ni zile ambazo miradi mikubwa ya kimkakati inatekelezwa kama vile TANESCO kupitia ujenzi wa mradi wa umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere katika Mto Rufiji na TRC ambayo inasimamia ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza.


Pamoja na Spika kuagiza viongozi hao kuitwa, tayari serikali ya awamu ya sita imeshaanza kuchukua hatua dhidi ya baadhi ya viongozi wa taasisi hizo. Moja ya mashirika hayo ni Shirika la Posta Tanzania ambalo tayari bodi ya wakurugenzi imevunjwa na uteuzi wa ofisa mtendaji mkuu kutenguliwa.

Ni vyema baada ya wakuu wa taasisi hizo pamoja na viongozi wa bodi kuitwa na kuhojiwa, ni vyema mamlaka za uteuzi kuwachukulia hatua dhidi yao pamoja na kuvunja bodi za wakurugenzi kutokana na kushindwa kusimamia na kuzishauri menejimenti za mashirika hayo.

Tunasema hivyo kwa sababu siku zote bodi za wakurugenzi zimepewa mamlaka ya kusimamia menejimenti za mashirika kuhakikisha zinafuata na kutekeleza maagizo yote yanayotolewa katika uongozi bora wa taasisi husika.

Ni imani kwamba kwa kuwawajibisha wakurugenzi hao wa bodi za mashirika na menejimenti zao, nidhamu kwa watendaji wa mashirika na taasisi za umma itarejea na watu watawajibika ipasavyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wanufaika mikopo ya elimu ya juu, serikali sasa imesikia kilio chenu

Na Sabato Kasika

**SASA** ni wazi kwamba msuguano kati ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na wanufaika wa mikopo ya bodi hiyo na hata wanafunzi wapya utakuwa umekwisha.

Baadhi ya wanufaika wamekuwa wakilalamikia madeni kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka na kusababisha ugumu wa kumaliza kuyalipa hadi pale washurutishwe na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Wakati hao wakilalamikia kuongezeka kwa madeni asilimia sita kila mwaka, wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu, nao hudai kukosa mikopo inayotolewa na bodi hiyo, hali ambayo husababisha msuguano kati yao na HESLB.

Hata hivyo, inawezekana msuguano huo ukaisha, kutokana na hatua zilizochukuliwa na serikali za kufuta baadhi ya tozo zilizokuwa zikilalamikiwa na wanufaika wa elimu ya juu.

Akihutubia katika kilele ya Siku ya Wafanyakazi Duniani jijini Mwanza hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan, alitangaza kufuta ongezeko la asilimia sita kila mwaka katika deni la wanufaika wa mikopo hiyo.

Wakati serikali imetengaza kufuta asilimia hiyo, imeendelea kusikia kilio cha wanufaika wa mikopo hiyo kufuta pia tozo ya adhabu ya asilimia 10 iliokuwa ikitozwa kwa wanufaika wanaochelewa kulipa mikopo ya elimu ya juu.

Hatua hiyo imetengazwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, ikiwa ni siku chache tangu Rais Samia afute ongezeko la asilimia sita ya mkopo huo kila mwaka ili kulinda thamani ya fedha.

Ninaamini kwamba, hatua zilizochukuwa na serikali, ni wazi manung'uniko na malalamiko ya muda mrefu ya wanufaika wa mikopo hiyo vitakuwa vimekwisha na kuwafanya walipe madeni yao bila kushurutishwa.

Kwa kuwa asilimia sita na hiyo 10 ya kuchelewa kulipa mikopo, vimeondolewa, ingependeza wanufaika ambao wako kwenye ajira, kuhakikisha wanalipa madeni yao kwa wakati wahitaji wengine wanufaike.

Iwapo wanufaika watalipa madeni yao kwa wakati, hatua hiyo itasaidia wanafunzi wapya wanaojiunga na vyuo vikuu wapate mikopo kwa wakati ili kuondoa msuguano kati yao na bodi husika.

Asilimia sita ya kila mwaka imefutwa, inawezekana sasa madeni hayatoengezeka, ambayo baadhi ya wanufaika wakidai kuwa yalikuwa hayalipiki kutokana na ongezeko hilo.

Kwa kuwa sasa visababishi vilivyokuwa vikichangia kuwapo kwa msuguano vimeondolewa, kilichobaki na wahusika kutimiza wajibu wao, wakitambua kuwa dawa ya deni ni kulipa.

Wakumbuke kuwa, hatua zilizochukuliwa na serikali zitakuwa zimewapunguzia mzigo ambao kwa muda mrefu walikuwa wakiulalamikia na kusababisha washindwe madeni yao kwa wakati.

Vilevile kulipa madeni yao kwa wakati kutakuwa kumeisaidia bodi kukusanya fedha za kutosha, na hivyo kuwezesha wanafunzi wapya wanaojiunga na vyuo vikuu nchini kupata mikopo bila usumbufu.

Ikimbukwe kwamba, kila mara kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wanafunzi wapya wanaojiunga na vyuo vikuu wakidai kukosa mikopo inayotolewa na bodi hiyo.

Mbali na hao, wengine katika muhula wa kuanza masomo, hulalamikia kutowekwa kwenye orodha ya wanatakaopata mikopo licha ya kuwa kwenye fani ambazo zinazotajwa na serikali kuwa zitapewa kipaumbele.

Inawezekana baadhi ya wanufaika wa mikopo kuchelewa kulipa madeni yao kwa wakati kumechangia kuwapo kwa hali hiyo, sasa kwa kuwa serikali imesikia kilio chao, si vibaya wakaanza kulipa kwa wakati.

Kila upande ikitumiza wajibu wake ipasavyo, ninaamini kwamba hakutakuwa na manung'uniko kutoka kwa wanufaika wa mikopo au wanafunzi wapya kuelekeza kwenye bodi hiyo.

Wanuifaka wakilipa madeni yao kwa wakati bila shuruti, inawezekana ikasaidia bodi kuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya wanafunzi wapya wanaotakiwa kunufaika na mikopo hiyo.

HESLB iliwahi kuweka wazi kwamba, lengo la tozo ya asilimia sita lilikuwa ni kuiwezesha Serikali, kupitia bodi hiyo kuwa na mfuko endelevu kukopesha wahitaji wengine bila kuathiri thamani ya fedha za mkopo ambazo mnufaika alipokea akiwa masomoni.

Kwa hali hiyo, kuna umhimu wa kila mnufaika kurejesha mkopo wake kwa wakati, lakini pia kufutwa kwa asilimia 10 iliyowagusa wacheleweshaji wa mikopo kusiwafanye wanufaika kubweteka.

SAFU

AFYA

# Faida kedekede za kitunguu maji kwa afya ya mwanadamu



**Na Mwandishi Wetu**

KITUNGUU maji ni aina ya mboga yenye harufu kali inayochangamsha mwili. Pia kitunguu ni kiungo ambacho kina virutubisho katika vyakula na kuvifanya viwe na ladha nzuri.

Nchini Tanzania, kiungo hicho ni maarufu na kunazalishwa katika mikoa mingi ikiwamo ya Morogoro, Iringa na Arusha ambayo ina rutba nzuri.

Kwa kawaida, watu wengi wamekuwa wakikitumia kila siku katika kuunga na vyakula mbalimbali hususan mboga au kachumbari na saladi. Ni nadra kiungo hicho kukosekana ndani ya nyumba kutokana na umuhimu wake hasa katika kutia nakshi mboga ya aina yoyote.

Pamoja na matumizi ya kila siku kwa chakula, watu wengi hawaelewi manufaa ya kiafya yaliyomo ndani ya kitunguu maji. Lakini wataalam wanabainisha kuwa kuna manufaa makubwa kwa kutumia kiungo hicho.

Mbali na kutumika kama kiungo katika mboga, kitunguu maji kinaweza kutengenezewa juisi kwa kukikatakata ma kisha kukisaga kwa blenda kwa kuchanganya na maji ya kunywa.

Kwa kufanya hivyo, inaelezwa kuwa mtu anapojisikia vibaya hasa kwa watu ambao wanasumbuliwa na kifua mara kwa mara, suluhisho la tatizo lao ni juisi ya kitunguu maji.

Kwa mujibu wa wataalam wa afya, kiungo hicho kimekuwa kikitibu na kuponya maradhi mbalimbali kutokana na kuwa na salfa ambayo ni nzuri, ikiwamo katika kupambana na maradhi ya ini. Pia inaelezwa kuwa husaidia kuponya kansa kwenye utumbo na kinywa kutokana na kuwa na virutubisho vingi vya vitamini C.

Sambamba na maradhi hayo, kitunguu maji kina kazi nyingi katika mwili wa binaadamu, kwani hutibu magonjwa mbalimbali. Hii inatokana na kuwa chanzo cha madini mengi ambayo yanapatikana katika kiungo hicho ambayo yana umuhimu mkubwa katika mwili wa binaadamu.

Licha ya kuwa na umuhimu huo, pia huimarisha afya ya moyo, kuzuia kansa, huukinga mwili dhidi ya vidonda vya tumbo, huongeza joto mwilini na huzuia vimelea vya magonjwa mbalimbali katika mwili wa binaadamu.

Aidha, inaelezwa kuwa faida za kitunguu maji katika mwili wa binadamu ni pamoja na kuupa mwili nishati, kuongeza nguvu, huimarisha misuli ya mwili, huongeza hamu ya kula, hulainisha tumbo na kuondoa tatizo la kukosa choo.

"Faida nyingine ya kitunguu ni kuwa kinatibu pumu, uvimbe wa pafu, saratani, majipu, mvilio wa damu, kufungua choo, kupunguza uzito na chunusi," inabainisha taarifa ya kitalaamu kuhusu manufaa ya kitunguu.

Pia inabainishwa kwamba kitunguu maji kina kemikali ambazo zinasaidia kazi ya Vitamini C katika mwili wako, hivyo kukuongezea kinga ya mwili. Pia kina kemikali aina ya chromium ambayo inasaidia kudhibiti sukari katika damu.

Kutokana na umuhimu wake kwa afya ya binadamu, kwa karne nyingi, vitunguu maji vimekuwa vikitumika kupunguza uvimbe na kuponya maambukizi.

**AFYA YA MOYO, SARATANI**

Kama ilivyoelezwa, vitunguu maji vimekuwa vikitumika kwa wingi katika chakula na watu hufurahia kuwamo kiungo hicho katika kila mlo. Lakini habari njema ni kwamba vitunguu vibichi vinasaidia kutegeneza lehemu nzuri, hivyo kuufanya moyo kuwa na afya njema.

Pia kemikali yenye nguvu iitwayo 'quercetin' katika vitunguu maji inaelezwa kuwa husaidia kwa kiasi kikubwa kuzuia saratani mbalimbali katika mwili wa binadamu.

Kwa wale ambao wamekuwa wakisumbuliwa na sumu ya nyuki kutokana na kuumwa mara kwa mara, hii ni habari njema. Mtu akiwa ameumwa na nyuki, anashauriwa kuweka juisi ya kitunguu maji katika sehemu iliyong'atwa, hivyo kusaidia kupata nafuu ua maumivu na uvimbe kutowasha.

Licha ya faida hizo, kitunguu maji kinaelezwa kuwa ni kiboko katika kukabiliana na tatizo la vidonda vya tumbo. Kwa mantiki hiyo, utumiaji wa mara kwa mara wa vitunguu maji katika namna yoyote husaidia kudhibiti tatizo hilo.

**KUPAMBANA NA TB**

Utafiti mbalimbali wa kisayansi unaonyesha kwamba juisi ya kitunguu maji ina uwezo wa kuua vijidudu vinavyosababisha maradhi ya kifua kikuu. Inabainishwa kwamba juisi hiyo huua vijidudu hivyo baada ya mgonjwa kunusa moshi wake.

Sambamba na hiyo, kitunguu maji huongeza hamu ya kula. Kikifanywa kuwa achari, ukali wake hupungua huongeza mno hamu ya kula. Pia kikiliwa kikiwa kimechomwa huongeza nguvu na nishati mwilini na huimarisha misuli ya mwili.

Aidha, kitunguu maji kikipikwa na kuliwa pamoja na samli, husaidia kuongeza nguvu za kiume pamoja na kuboresha nguvu za kiume. Pia kikitengenezwa supu pamoja na nyama, huongeza hamu ya tendo la ndoa kwa wanawake.

Kwa upande wa wanawake ni habari njema kwao kiafya iwapo wanatumia vitunguu mara kwa mara. Hii ni kutokana na taarifa kwamba Kitunguu maji hutumika kutibu tatizo la kukosa hedhi kwa wanawake.

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Kula kwa mirija nako ni kula



**Na Joseph Kulangwa**

KIUMBEHAI chochote ili kuishi kinahitaji kula. Mti, jani, mdudu, ndege, mnyama na binadamu ni viumbe hai. Viumbe hawa wasipokula kwa muda fulani hupoteza maisha.

Ulaji wa viumbe hawa hutofautiana, wengi hutumia kinywa chenye ulimi na meno, vingine havina meno na vingine hutumia midomomirija na vingine mizizi. Hivyo chakula ni muhimu.

Binadamu hujishughulisha kupata chakula chake, kwa kufanya kazi au kuzalisha chakula mwenyewe shambani mwake, huku wanyama na ndege wakiwinda na kuokoteza, mimea inafyonza ardhini ilikoota.

Binadamu na mnyama wana aina mbili za kula; kwanza wanaweza kutumia vinywa vyao na wakati mwingine vinywa vikiwa na matatizo, hula kwa mirija inayopitishwa puani au sehemu nyingine ya mwili.

Si mara chache kushuhudia mnyama au binadamu aliyelazwa hospitalini akiwa amewekewa mirija ya chakula puani, au kupitia matundu aliyotobolewa mwilini wake.

Ulaji wote huo humwezesha mlaji kupata lishe na kuendeleza uhai wake. Hivyo njia hizo mbili ni halali, zinazokubaliwa kutumika kuingiza chakula mwilini na kuwezesha maisha ya kiumbe husika.

Nautumia mfano huu nikirejea hotuba ya Rais Samia Suluhu Hassan katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani-Mei Mosi, yaliyofanyika kitaifa mkoani Mwanza.

Kabla ya siku hiyo, wafanyakazi walikuwa na shauku ya kumsikia Rais wao mpya, kwa mara ya kwanza akiwahutubia katika sherehe hizo, huku pia wakitarajia kusikia kauli njema kutoka kwake.

Wafanyakazi hao walikuwa wakisubiri kumsikia Rais akiongeza mishahara, baada ya kukaa miaka sita (sekta ya umma) na miaka minane (sekta binafsi) bila kuongezwa.

Mazingira yalikuwa hivyo kutokana na Serikali ya Awamu ya Tano, kujiegemeza zaidi katika kutekeleza miradi yake ya kimkakati na kuwasahau wafanyakazi ambao kila ilipofika Mei mosi, walidhani mambo yangekuwa mazuri.

Lakini hadi awamu hiyo inaondoka baada ya kifo cha Rais Dk John Magufuli, hawakuwa wameongezwa mishahara, lakini kuingia kwa Rais Samia kulionekana kuwapa faraja na matumaini makubwa hasa kutokana na kauli zake.

Rais katika hotuba zake za awali, alionekana kuguswa na maisha ya Watanzania, na kuelezea dhamira yake ya kuhakikisha uchumi unakua na wananchi wanaondokana na ugumu wa maisha, ambao ulishazoeleka licha ya kilio cha muda mrefu.

Kwa kuwa wafanyakazi hao walitarajia kuwa huenda Rais angetoa 'NENO' (nyongeza ya mishahara), lakini 'akaongeza mishahara' kwa njia tofauti, yaani badala ya kulisha kwa kinywa, akalisha kwa mirija.

Rais aliamua kupunguza maumivu kwa wafanyakazi, kwa kupunguza kodi ya mishahara ya Lipa Daima Unavyopata (PAYE) kutoka asilimia tisa hadi nane na kufuta tozo ya asilimia sita kwa mikopo ya elimu ya juu.

Ipo mifano ya kuthibitisha hilo, kwamba kwa mtumishi wa umma anayepata mshahara wa Sh. 500,000 bila kuwa na makato mengine ya lazima kama ya mfuko wa hifadhi ya jamii, kwa nafuu hiyo ya PAYE, mshahara wake utaongezeka kwa Sh. 2,300 kwa mwezi sawa na Sh 27,600 kwa mwaka.

Mtumishi kutokana na hatua hiyo, atakuwa anakatwa Sh. 18,400 badala ya Sh. 20,700 katika mshahara wake kwa mwezi. Lakini nafuu kubwa itaonekana kwa mwenye mshahara mkubwa.

Rais Samia aliahidi, kuwa kutokana na yeye kutokuwa Ikulu kwa muda mrefu, hatua inayoonesha anajipanga kwa kupitia makabrasha aliyoyakuta, na ushauri kutoka kwa wasaidizi wake, ifikapo Mei mosi, mwakani, ni dhahiri atapandisha mishahara.

Kama alivyojitanabaisha kama "mfanyakazi mwenzenu", anapata uchungu kama walivyo wafanyakazi wengine, hivyo kuona umuhimu wa kukomesha kilio cha muda mrefu cha wafanyakazi.

Ingawa wafanyakazi waliondoka kinyonge kwenye uwanja wa CCM Kirumba, kwa niaba ya wafanyakazi wengine nchini waliokuwa na matumaini hayo, ni vema wakajenga imani kwa Rais huku wakijua, "Rais amewalisha kwa mirija" ili waishi hadi Mei mosi, mwakani "watakapolishwa kwa kinywa". **Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Vitisho kutaka kuuawa DED na Mbunge, RC, RPC wawajibike



Na Thobias Mwanakatwe

NENO Tishio linatafsiriwa kuwa ni hatari inayokaribia, inayotokea au tukio ambalo halijatokea bado.

Na kutishia vile vile ni kosa la jinai ambalo unapotishia kuua kwa maneno unakuwa umefanya kosa kwa sababu ni kinyume cha kifungu 89 (2)(a) cha Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 Mapitio ya 2002.

Katika Mkoa wa Songwe, suala la viongozi kutishiwa kuuawa na viongozi wenzao linaonekana kushamiri kama si kushika kasi hali ambayo kimsingi inawashtua sana wananchi wa mkoa huo.

Katika tukio la karibuni, Mbunge wa Songwe, Philip Mulugo, aliweka wazi kwenye kikao cha wadau wa ufuta kwamba Mkuu wa Wilaya (DC) ya Songwe, Samuel Jeremiah, ametishia kumuua.

Mulugo ambaye ni kipenzi kikubwa cha wananchi wa jimbo hilo na mkoa mzima wa Songwe ambao mara kadhaa katika uchaguzi mkuu wamekuwa wakimpitisha bila kupingwa kutokana na uchapa kazi wake makini, aliweka wazi hatari hiyo iliyoko mbele yake mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemus Mwangela.

Katika maelezo yake, Mulugo alitaja sababu za kutaka kuuawa na DC huyo kuwa ni pamoja na kumfuatilia DC kuhusu fedha zinazotolewa na wawekezaji wa maendeleo wilayani humo yakiwamo makampuni makubwa ya uchimbaji wa madini na wachimbaji wadogo.

Pia mbunge anapofuatilia fedha za michango ya wananchi wake pale wanapoamrishwa kuchangia miradi ya maendeleo mfano ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na kituo cha afya cha Mbuyuni.

Aidha, chuki ya mkuu wa wilaya dhidi ya mbunge huyo zinadaiwa ni kutokana na mbunge huyo ambaye ni mwakilishi wa wananchi anapopata malalamiko mengi kutoka kwa wafanyabiashara wanaodaiwa kutoa fedha kwa vitisho ili kuogopa kufungiwa biashara zao na DC.

Mulugo pia alisema vitisho dhidi yake pia vimetokana na yeye (mbunge) kuwa mstari wa mbele kuwatetea wakulima wa ufuta ambao walisema hawako tayari kwa sasa kupeleka mazao yao kuuza kwa mfumo wa stakabadhi ghalani uliokuwa umetangaza na serikali ya wilaya.

Mulugo akamalizia kusema kuwa RC ndo analea mambo haya kwa kutochukua hatua dhidi ya DC ambaye amekuwa hana ushirikiano na viongozi wenzake na hata viongozi wa chama wamefanya kila jitihada kupeleka barua kwa RC lakini amefumba macho.

Cha kushangaza siku chache baada ya mheshimiwa Mulugo kulisema hilo hadharani, Jeshi la Polisi kupitia kwa Kamanda wa Mkoa likaibuka na kutoa taarifa kuwa limemwita DC huyo kumhoji kuhusiana na kudaiwa kutishia kumuua mbunge. Lakini swali ni kwamba jeshi hilo lilikuwa wapi siku zote wakati jambo hilo limetokea siku nyingi.

Tukio lingine ambalo nalo lilileta msisimko na taharuki ni tishio la Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mbozi, Hanji Godigodi, ambaye naye anadaiwa alitishiwa kuuawa.

Godigodi anadaiwa kutishiwa kuuawa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Songwe, Henerico Mkola, mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe na Katibu Tawala wa Mkoa huo.

Sababu za mkurugenzi huyo kutishiwa maisha ni baada ya kukataa kuidhinisha malipo ya Sh.milioni 12 alizotakiwa kulipwa Mwenyekiti huyo wa CCM baada ya kudaiwa kusambaza vifaa vya ujenzi nondo na saruji.

Mkurugenzi alikataa kulipa fedha hizo licha ya kupewa agizo mara tatu na RC kwa sababu inasemekana vifaa anavyodai kuvisambaza Mwenyekiti wa CCM havikupelekwa kwenye ujenzi wa mradi wowote wa halmashauri na badala yake vilipelekwa kwenye ujenzi wa jengo moja la kiongozi mmoja wa serikali mkoani humo.

Kwa msingi huo, utaona mkurugenzi alikuwa na hoja ya msingi kukataa kuidhinisha malipo hayo ya Sh. milioni 12, lakini cha kushangaza ameandamwa na madiwani ambao walifikia hatua ya kutoa tamko la kususa kufanya naye kazi.

Kitendo cha madiwani kumwandama mkurugenzi huyo kinaonyesha dhahiri kuwa wameungana na Mwenyekiti wa CCM, RC na RAS kutaka kumsulubu mtendaji huyo wa halmashauri.

Kutokana na mfululizo wa matukio haya ya mbunge na DED kutishiwa kuuawa, binafsi naona kuna tatizo kwa viingozi wakubwa wa mkoa huo kwa maana ya RC na RPC.

Kama RC na RPC wangekuwa makini kushughulikia matatizo haya kwa wakati yasingekuwa makubwa na kwa mantiki hiyo naona viongozi hawa wanapaswa kuwajibika kwani wameshindwa kufanya kazi yao.

RC ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa alipaswa kuyashughulikia matatizo haya kwa uharaka kabla ya kutoka kwenye 'public' lakini hajafanya hivyo na hapa ndipo napoona umuhimu wa yeye kutakiwa kuwajibika.

Kuendelea kwa viongozi kulumbana na kutishiana maisha kunadhoofisha maendeleo katika mkoa huo na hivyo Rais mama yetu Samia Suluhu Hassani litazame hili la mkoa was Songwe na ikikupendeza safisha viongozi hawa wasiowajibika ili kazi iendelee.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU UBARIKI MKOA WA SONGWE**

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com.**

## DARASA LA NDOA

# Uwapo wa ndoa imara chachu ya maadili mema katika jamii



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

**Mume na mke ni watu muhimu katika kujenga familia na jamii iliyo bora. Wazazi wanaposhindwa kuwa mfano mwema kwa watoto wao, hali hii huathiri sana makuzi yao. Wazazi wanapotimiza majukumu yao ipasavyo, wanaweka msingi imara wa nidhamu na maadili mema kwa watoto wao.**

TUNAISHI katika jamii inayobadilika kwa kasi ambapo tunashuhudia mmomonyoko mkubwa wa maadili. Vitendo vya ubakaji, ukatili wa kijinsia, kuvunjika kwa ndoa, vijana wengi kuishi kinyumba kabla ya ndoa, kutokuheshimu na kutokujali wazee, ubinafsi, uvivu, wizi na uporaji ni baadhi ya vitendo ambavyo vinashamiri katika jamii yetu.

Vijana wengi wanaooa na kuolewa leo baadhi yao wameshindwa kuwa baba na mama bora katika familia zao. Wengi wao hawajitambui wao kuwa ni nani na hawajui wajibu wao katika familia kuwa ni upi.

Miongoni mwa sababu zinazochangia tatizo hili, kwanza, ni ukosefu wa ufahamu na maarifa ya kutosha kuhusu taasisi ya ndoa, pili, makuzi wakati wa utoto. Watoto wengi wa leo hawafundishwi stadi za kazi za maisha katika ngazi ya familia. Wengi wao wanalelewa kama kuku wa kizungu au kisasa.

Hali kadhalika, wengi wao wana uzoefu mbaya kutoka kwa wazazi wao (negative parenthood). Wazazi wengi hawana muda na watoto wao. Wazazi wengine ni watu wa ugomvi kila siku na huhamishia matatizo yao kwa watoto; watoto hawajawahi kuona matendo ya upendo ya wazazi wao. Hali hii imesababisha wazazi wengi kupoteza sifa ya kuwa kielelezo kizuri (role model) kwa watoto wao.

Baadhi ya watoto wamerithi maumivu na mambo mabaya zaidi kutoka kwa wazazi wao kuliko mambo mazuri. Matokeo yake nao wanafanya vivyo hivyo wanapokuwa watu wazima kwa kuamini kuwa ndio mtindo wa maisha, kwani ndicho walichokiona na kujifunza kutoka kwa baba na mama yao.

Mume na mke ni watu muhimu katika kujenga familia na jamii iliyo bora. Wazazi wanaposhindwa kuwa mfano mwema kwa watoto wao, hali hii huathiri sana makuzi yao. Wazazi wanapotimiza majukumu yao ipasavyo, wanaweka msingi imara wa nidhamu na maadili mema kwa watoto wao.

Nidhamu na maadili mema hujengwa pale baba na mama wanapopendana, wanaposikilizana, wanaposaidiana, wanaponia mamoja, wanapochukuliana katika raha na shida, wanapopata muda wa kuwa na watoto wao na kuwafundisha stadi za kazi na maisha; wanapowaonya na, kuwarekebisha wanapokosea, wanapowaadibisha kwa upendo, wanapoweka kanuni na miongozo mbalimbali ya kusimamia familia ili kujenga familia imara. Wazazi wanapowajibika kwa watoto wao wanaongeza thamani yao kwao.

Wazazi wakati mwingine tumewakosea watoto wetu. Matokeo yake tunawalaumu na kuwalaani kwa makosa yetu wenyewe pale wanapokuwa na maadili potofu na wanaposhindwa kuwajibika ipasavyo kwetu. Ni muhimu mzazi kujifanyia tathmini binafsi kwa kurudi nyuma na kuangalia mahali ulipokosea na kuanguka.

Inawezekana badala ya kulaumu na kulaani watoto au mtoto wako, utajikuta unapaswa kuomba msamaha kwa Mungu na watoto wako kwa kuwakosesha, kwani hicho kinachokutokea leo ni matokeo ya ulichowekeza wakati wa utoto wao. Ni ushauri wangu kwamba, hali ya namna hii inapojitokeza, jambo la msingi ni kutengeneza mambo yako na watoto wako ili maisha yawe shwari na si shari kwa kuwa kulaumu na kulaani hakutasaidia kuondoa tatizo.

Kila mzazi atavuna alichopanda kwa mtoto au watoto wake. Ukipanda mema, utavuna mema na ukipanda mabaya, utavuna mabaya. Inawezekana athari usizione leo, bali utaziona hapo baadaye. Watoto waliolelewa vibaya hawako salama sana, kwani dhamiri zao zinakuwa butu kukabiliana na changamoto na mazingira tofauti.

Malezi bora hujenga dhamiri imara na misuli kwa watoto ambayo itawawezesha kujisimamia na kujitawala katika maisha yao. Kwa mantiki hii,wazazi wajifunze kuwekeza malezi bora kwa watoto wao ili kuepuka maumivu na majuto leo na hapo baadaye, kwani wahenga wanasema, mtoto umleavyo, ndivyo akuavyo.

Nyumba ni mahali pa malezi na kutoa mafunzo ya maadili na mwenendo mwema kupitia mfano na mafundisho ya wazazi. Nyumba si jengo tu watu wanamokaa, bali ni mahali pa faraja, starehe na kushiriki amani na furaha. Familia ni taasisi ya kuadibisha na shule ya kwanza ya mafunzo kwa watoto, ambamo raia wema, waumini, viongozi, waume na wake bora hutengenezwa.

Ni rahisi sana kubadili au kurekebisha kitu kwenye umri wa utoto kuliko akiwa mtu mzima, sawa na usemi wa Wahenga usemao, mkunje samaki angali mbichi. Kwa kufanya hivyo, wazazi watakuwa wanajenga nguvu kazi imara na kizazi chenye baraka katika familia, jamii na taifa.

Ndoa ni kitovu cha familia na malezi na zawadi ya Mungu kwa mwanadamu. Familia ndio msingi wa maadili mema kwani tabia na mienendo yetu hujengwa katika familia. Hivyo, ili tuwe na wanajamii na viongozi waadilifu, lazima mkazo uwekwe katika malezi ngazi ya familia. Ndoa zikiwa imara, tutakuwa na familia, jamii na taifa imara. Maendeleo ya taifa na maadili mema katika jamii yanategemea ndoa imara kwa kuwa katika ndoa ndiko watu wanakotengenezwa.

Msisitizo wa Rais wetu, Samia Suluhu Hassan, kuhusu malezi bora na kujenga msingi wa maadili mema kwa watoto wetu, alipokuwa akihutubia Mkutano wa Wazee Mei 7, 2021 mkoani Dar e Salaam ni jambo muhimu la kuzingatiwa na linalohitaji kufanyiwa kazi kwa dhati kuanzia ngazi ya familia. Kwa kufanya hivi, tutakuwa tunashughulika na kiini cha ugonjwa badala ya kushughulika na dalili zake.

**Mungu ibariki Tanzania! Kazi ya malezi bora iendelee!**

**• Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

Mei 9, 2021
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
*Jumapili*



ILIKUWA SIKU YA FURAHA NA NDEREMO, WAKATI BWANA MBURUJA MMBATA NA IRENE MNGAZIJA WALIPOFUNGA NDOA APRILI 18, MWAKA HUU JIJINI TANGA NA KUFUATIA SHEREHE YA KUWAPONGEZA.

## HARUSI

Ukurasa 12



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Umuhimu wa malighafi bora katika ujenzi nyumba imara

## VIPAPATIO VYA KUOKA

Ukurasa 14





# BAKI
## NA RANGI YAKO

Ukurasa 14

# Binti katumwa ukindu,karudi mikono mitupu

**Beatrice Moses**

ASUBUHI moja nikiwa nimeamka, ghafla nilimsikia jirani yangu akilalamika mtoto wake Fatuma, alivyokuwa mzembe na mbumbumbu wa mambo.
Kwa hasira alisikika akimsema iweje jana yake amemtuma ukindu wa kusukia ukili, akamrudi mikono mitupu.
Kilichomuuma sana ni baada ya binti yake kujibu kirahisi kuwa hakuna ukindu anaousema, ikiwa jana yake alipita hapo sokoni na kuona watu wakiuza kwa mafungu.
Kutokana na kile nilichokisikia, ndipo nilipowaza jinsi wazazi na walezi walivyojisahau kudumisha jukumu letu la kuhakikisha watoto wanakuwa na kuendeleza mambo mazuri ikiwamo ubunifu wa kiasili.
Nimejaribu kufuatilia baadhi ya bidhaa ambazo zinaweza kuwa hatarini kutoweka kuwa ni pamoja na zile zinazotengenezwa kwa kutumia ukindu.
Ukindu linaweza kuwa ni neno geni kwa baadhi ya vijana wa kizazi cha sasa, yawezekana kutofahamu malighafi hiyo inatokana na mazingira na makuzi aliyolelewa.
Ukindu ni malighafi ya asili hutumika kutengeneza mikeka, vikapu, mikoba, kawa na vibwaya vya wacheza ngoma ambapo huvutia kuwatazama kutokana na jinsi wanavyocheza kwa kutingisha na kufanya uchanue na kupepea.
Nakumbuka ningali msichana mama alikuwa akinituma kumnunulia ukindu, pia alikuwa na utaratibu wa kunitengenezea wangu na kunifunza jinsi ya kusuka ukiri.
Kazi ya kuunganisha ukindu wenyewe kwa wenyewe hufanywa kisha baada ya kukamilika unaweza kuupaka rangi maalumu ipendayo baada ya hapo ndipo unashona bidhaa uitakayo mkeka au kikapu.
Nimejiuliza mengi kulingana na malezi yetu ya sasa ni wazi kwamba kuna ujuzi ambao unaweza kupotea hivyo bidhaa za asili kama hizo zinazotengenezwa kwa ukindu zikatoweka kabisa.
Bidhaa hizo ni miongoni wa vivutio vya utalii, pia zinatambulisha utamaduni wetu kwa wageni, ambao ni wazi kwamba unaweza kupotea kutokana na kukua kwa teknolojia ambayo pia inachochea kubadilika kwa mfumo wa malezi.
Ni wajibu wa wazazi, walezi na taasisi husika kuhakikisha tunaendelea kudumisha ujuzi wa utamaduni ambao licha ya kuwa unatumika na wanaoutambua kama ajira lakini pia bidhaa hizo zinavutia na ni rafiki wa mazingira.
Bidhaa hizo hutumika na watu wa jinsi na rika tofauti, kofia pia ni miongoni mwa kivutio, husaidia kuzuia mvaaji kuunguzwa mionzi ya jua.
Hivi karibuni serikali imeendelea na juhudi zake za kupinga matumizi ya mifuko ya plastiki, ambayo licha ya kuchafua mazingira kutokana na kutupwa ovyo lakini pia ni hatari kwa baadhi ya mifugo.
Bidhaa iliyotengenezwa kwa ukindu licha ya kuwa hutumika kwa muda mrefu kutegemea na utunzaji, hata wakati inapochaka ni salama kuiteketeza za kwa kuichoma moto kwa kuwa moshi wake huna kemikali, lakini pia ikifunikiwa uoza tofauti na mifuko ya plastiki.
Hivyo pamoja na kukuwa kwa teknolojia wazazi na walezi ni vyema kuhakikisha kuwa katika maeneo ambapo jamii yao kuna tamaduni zinazotambua umuhimu wa bidhaa zinazotengenezwa kwa ukindu zinaendelezwa kizazi kwa kizazi.

## NA HAMIS KIDAGO

0657 207168

# QUIZ

### LE QUIZ DU WEEK

L'Adjectif Qualificatif – Vivumishi vya sifa

Geuza vivumishi vya sifa vifuatavyo ambavyo viko katika jinsia ya kiume au masculin kwenda jinsia ya kike au féminin.

Mfano – Jeune – jeune

Grand – grande
Brun – brune
Distingué – distinguée
Charmant – charmant
Privé – privé
Tranquille – tranquille
Fragile – fragile
Solide – solide
Lourd – lourde
Confortable – confortable
Petit – petite
Joli – jolie
Original – originale
Agréable – agréable
Content – contente
Connu – connue

Muhimu:Vivumishi vya jinsi ya kiume vinavyoishia na herufi e hubadilika kuwa vya jinsia ya kike kwa kuongeza herufi e nyingine. Ingawa sio kwa maneno yote. Mfano distingué (masculin) – distinguée (féminin) lakini tranquille (masculin) na tranquille (féminin).

Chagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano.

Dans la cuisine
C'est un repas froid.
Attention! l'assiette (fs) est chaude.
Cette viande est très salée.
C'est une sauce sucrée?
Le gâteau est trop cuit.
La cuisson est parfaite.
Le jus d'orange est glacé.
Voici une salade verte.
C'est un plat épicé.
Cette recette est excellente.

Weka jibu sahihi kutoka kwenye mabano.

J'ai dessiné...
Une maison grise.
Le ciel bleu.
La pelouse verte.
Un oiseau noir.
Un arbre très haut.
Et un grand soleil.

Chagua kutoka kwenye mabano neno sahihi.

Une journaliste espagnole.
Un artiste japonais.
Un photographe allemand.
Une rédactrice chinoise.
Un dessinateur polonais.
Une correspondante mexicaine.
Un reporter argentin.
Une actrice américaine.

Geuza maneno yafuatavyo kuwa katika jinsi ya kiume umoja.

Mfano: une rue étroite – un chemin étroit.
Une place animée – Un parc animé.
Une grande avenue – un grand boulevard.
Une entrée large – un troittor large.
Une place tranquille – un jardin tranquille.
Une petite impasse – un petit passage.
Une rue agréable – un quartier agréable.

Badili kama inavyoelekezwa kwenye mfano.


Mfano: Un garcon blond – une fille blonde.
Une femme brune – un home brun.
Une voisine bruyante – un voisin bruyant.
Un enfant bavard – une dame bavarde
Une jeune fille charmante – un monsieur charmant
Un professeur passionant – une personne passionante.
Un homme âgé – une femme âgée.

Pigia stari jibu sahihi katika sentensi zifuatazo.


C'est une belle table.
Je dois acheter un nouveau stylo.
Ce tableau est faux.
C'est une idée folle.
Vous avez un beau chapeau.
Cet home est fou.
La température est vraiment fraîche.
C'est une jolie femme rousse.
Son mari est vraiment jaloux.
Ce voyage a été très long.

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA KIDOGO



Zao la mtama linahimili hali gani ya hewa?

MAMA mwenye nyumba alitaka kupandisha kodi, lakini kutokana na ubabe wa wapangaji wake alitafuta mbinu ya kuwaambia.

Mama: Wanangu leo nataka nizungumze na nyinyi

Mpangaji: Kuna nini tena?.. Tuambie tu

Mama: Askari walinifuata wakaniambia humu ndani kuna majambazi, hivyo nataka kubomoa nyumba yangu

Mpangaji: Sisi sio majambazi, ila huko kubomoa nyumba sisi tutakwenda wapi?

Mama: Kila mtu aende alipotoka, labda kwa kuwahurumia nawapa muda wa mwaka mmoja lakini kodi inapanda hadi 40,000

Mpangaji: Tulikuwa tunakuangalia tu, tayari mwanao katuambia kila kitu.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# 'Nguvu ya marafiki nilijikuta kwenye madanguro, sasa natamani kuokoka'

KARIBU tena msomaji wangu katika safu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Bado naperuzi anga la vijana wetu hasa eneo la marafiki. Wiki iliyopita nilimjadili binti anayetaabishwa na tabia ya rafiki yake wa kike ya kutoka na mchumba wake.
Anasema amewekeza sana kwa mchumba wake huyo, lakini amebaini kupitia simu ya kiganjani ya mchumba kwamba ana uhusiano na rafiki yake huyo waliyeshibana. Hilo linampa wasiwasi sana, hivyo kujikuta njia panda asijue cha kufanya.
Katika makala ile, nilijaribu kuelezea rafiki ni nani na anaweza kukufanyia nini endapo hutakuwa makini.
Nilisema ukitaka kupata rafiki ni muhimu umpime kwanza, usiharakishe kumwamini maana yuko rafiki inampomfaa na siku ya taabu hayuko nawe kukusaidia.
Yupo pia rafiki abadilikaye kuwa adui, atazusha ugomvi ili kukuaibisha. Kumbe aliye rafiki yako ndiye anayeweza kukuangusha kwa kutumwa na shetani. Na ukweli ni kwamba adui yako ni yule aliye karibu yako, siku zote hatoki mbali.
Mbali na rafiki hao wabaya, wako walio waaminifu ambao mtu anapaswa kuwa nao.
Rafiki mwaminifu ana thamani kuliko chochote, hakuna awezaye kupima ubora wake.
Nikasema pia kwamba rafiki mwaminifu ni dawa itiayo nguvu mwilini. Watu wamchao Bwana hupata marafiki wa kweli, maana alivyo mtu, ndivyo na rafiki zake. Pamoja na hayo, neema ya Mungu ndiyo impayo mtu marafiki sahihi.
Msomaji wangu, kabla sijazama zaidi kuhusu balaa la marafiki, hebu tumsikie binti huyu ambaye marafiki walimpoteza akajikuta kwenye madanguro, na sasa anajuta akitamani kuokoka amche Mungu muumba wake.
Anasema hivi; "mama mimi naitwa Catty, naishi Mwanza. Umri wangu miaka 22. Nilikuwa nataka nifanikiwe kimaisha na kupata kazi. Naomba msaada".
Msomaji wangu, nilipousoma ujumbe huu kupitia simu ya kiganjani, ilibidi nimpigie simu niweze kumfahamu zaidi. Ndipo nikagundua mambo mazito aliyopitia hadi kufikia hatua ya kuomba msaada.
Katika maelezo yake akasema kwamba elimu aliishia kidato cha pili akaamua kwenda kuishi na marafiki zake waliomshawishi. Ni marafiki walioshindikana kwao, wengine wazazi wana maisha duni hivyo kulazimika kuingia mitaani kutafuta maisha.
Catty akasema hivi, "Wazazi wangu wana uchumi wa kawaida na waka hawakushindwa kunisomesha.
Ila mimi nilipomaliza tu kidato cha pili na kuingia kidato cha tatu, nilishawishiwa na rafiki yangu aitwaye Anna, badala ya kwenye shule tukawa tunazurura mitaani.
Nikawa natoka nyumbani kujifanya nakwenda shuleni, kisha nampitia rafiki yangu Anna kwao lakini hatuendi shuleni, tunakwenda mitaani na kujikuta tukiwa kwenye vilabu vya starehe usiku na kukutana na wanaume mbalimbali.
"Maisha yakawa hivyo na hatukurudi tena nyumbani.
Ni kunywa pombe, kuvuta bangi na madawa mengine ya kulevya, huku tukibadilisha wanaume. Ni maisha ya kutaabisha, ya mateso lakini kujinasua nikawa siwezi.
"Ni mwaka mmoja tokea niondoke nyumbani. Mama yangu akawa ananitafuta ndipo kaka mmoja anayeifahamu familia yangu akanikamata na kunipeleka kwa wazazi wangu. Hiyo ilikuwa salama yangu.
Mama aliponiona alilia sana, akaniambia niende kanisani ili neema ya Mungu ibadilishe maisha yangu.
"Sasa natamani sana kuokoka Mungu anisamehe na kuniongoza katika maisha yangu.
Niliwahi kwenda kanisani, nikaombewa mara moja sikurudi tena, nikaendelea na purukshani za starehe. Marafiki walikuwa sumu mbaya kwangu kwani nisingekuwa hapa nilipo", anamalizia kusema binti huyu akilia machozi kwenye simu.
Mpenzi msomaji, nimeeleza hapo awali kwamba rafiki unayemwamini anaweza kukuangusha. Kama rafiki hakupi wazo la kufanikiwa hakufai. Kama mama wa mtu alivyo, ndivyo na binti yake alivyo. Marafiki zako walivyo, ndivyo ulivyo. Huwezi kwenda zaidi ya rafiki zako.
Rafiki anayekwambia twende, disko, tukaibe na matendo mengine maovu, huyo siyo rafiki mzuri anakupoteza.
Lakini rafiki anayekwambia twende kwenye nyumba za ibada kupata mafundisho ya Mungu, huyo ni rafiki mzuri.
Rafiki ni yule anayekuinua mkono akupeleke juu, siyo yule anayekudidimiza. Maisha Ndivyo Yalivyo
**Msomaji wangu niishie hapa. Bila shaka umejifunza kitu hapo. Siku zote kuwa makini na marafiki. Je, una maoni au kisa cha kimaisha? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.**

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Tumuunge mkono Rais kulipa kodi kwa hiari

WIKI iliyopita, Rais, Samia Suluhu Hassan, alisisitiza umuhimu wa haki na kuahidi kuwa serikali haitakubali kodi ya dhuluma na kila mwananchi anawajibu wa kulipa kodi bila kulazimishwa.
Imani ya dini zote zinazungumzia haki na zaidi imefafanuliwa kuwa haki huinua taifa na siku zote taifa lenye viongozi wenye kutenda haki Mungu husikia maombi yao na kuyajibu.

Kauli ya Rais ni yenye tumaini kubwa na ameirudia kwa mara ya pili. Ya kwanza ni siku akiwaapisha makatibu wakuu na manaibu wao na alitumia nafasi hiyo kusisitiza kuwa serikali haitakubali kodi ya dhuluma.
Miaka ya hivi karibuni kilio cha walipakodi kilikuwa kikubwa kiasi cha wengi 'kuporwa' fedha zao kwenye akaunti kiasi cha wengi kukimbia nchi na kwenda kuwekeza kwingine.

Kutokana na hali hiyo, walioumia si serikali pekee kwamba ilikosa kodi, bali waliokuwa wameajiriwa na wategemezi wao walibaki bila kazi na kushindwa kupata mkate wa kila siku.
Lakini athari zilionekana zaidi katika mzunguko wa fedha. Zilipungua na watu kulijikuta hawana fedha mifukoni na hapo ndipo dhana ya maisha magumu ilipozidi kuongezeka kiasi cha wengine kuondoa watoto kutoka shule za binafsi kwenda za umma na wengine kufunga ofisi, kampuni na biashara mbalimbali.
Kwa kauli ya Rais Samia, maana yake anatambua madhara ya dhuluma ambayo yametajwa kwenye vitabu vitakatifu kuwa ya Kaisari (serikali) apewe Kaisari na ya Mungu apewe Mungu.
Sasa kwa utashi wa kisiasa uliopo maana yake Watanzania kila mmoja kwa nafasi yake anapaswa kufanya kazi kwa bidii, kulipa kodi zote za kisheria kwa wakati na usahihi ili kuijenga nchi kwa manufaa ya wote.
Ni muhimu tukamuunga mkono Rais Samia kwamba ameshaonyesha nia njema iliyojaa hofu ya Mungu ndani yake. Sasa nasi tumwogope Mungu kwa kutimiza neno lake kwa kuhakikisha kodi inalipwa kwa usahihi.
Manufaa ya kulipa kodi ni kuiwezesha serikali kujiendesha, kutekeleza miradi muhimu ya maendeleo ambayo itatunufaisha sote kwa pamoja na kulifanya taifa kuwa na uchumi mzuri na watu wake wenye furaha na amani. Pia huduma za kijamii kama elimu, afya na maji zinakuwapo kwa kiwango kikubwa.
Mathalani, mwezi ujayo itasomwa bajeti ya serikali ambayo itaonyesha mgawanyo wa keki ya taifa utakavyofanyika kwa kila Mtanzania.
Pia itaonyesha namna fedha zitakusanywa kutoka vyanzo mbalimbali.
Ni wajibu wa kila raia kulipa kodi na kufika mahali pa kuona aibu au kuumia moyoni pale ambako hujatimiza takwa ya Mungu, kwamba iliyo yake umpe na iliyo ya serikali ipeleke kwake.
Tulikipa kodi kwa usahihi maana yake uchumi utashamiri na ukiwa hivyo ajira zitaongezeka na maisha ya mtu mmoja mmoja yataboreka na Tanzania itapiga hatua kubwa kimaendeleo.
Na zaidi ni muhimu kwa mamlaka kusimamia sheria, kanuni na taratibu kwa kuwa zipo kwa ajili ya kuhakikisha wasiofanya kwa hiari wanalazimishwa kufanya hivyo.
Hakuna ubishi kuwa ili nchi iendelee ni lazima tulipe kodi, na hili litafanikiwa ikiwa kila mmoja kwa hiari yake atafanya hivyo.
Rais Samia kaonyesha njia, ni wajibu wa kila Mtanzania kumuunga mkono kwa kufanya kazi kwa bidii, uaminifu na kulipa kodi sahihi, wakati sahihi na kiwango sahihi ili maendeleo yawapo.
Aidha, ni muhimu kujiepusha na rushwa ambayo ni adui mkubwa wa taifa kwa kuhakikisha katika kulipa kodi kila mmoja anajiepusha kwa namna yoyote ile na rushwa ili kuchepusha kodi halali ya Kaisari.
Rushwa inachelewesha na kudumaza maendeleo, kwa kuwa hata haki haitapatikana kwa wakati kwa kuwa wapo watakaokosa haki yao kwa sababu tu ya rushwa na siku zote haki huinua taifa.
Rais Samia ametuaminisha ni muumini wa haki, basi nasi tumtendee haki kwa kulipa kodi stahiki, ili uendeshaji wa serikali uwe rahisi na maendeleo yaje kwa wote, na tukifanya hivyo tutakuwa tunaugusa Moyo wa Mungu kwa kuyaishi maandiko yake.
**Mungu ibariki Tanzania!**



ILIKUWA SIKU YA FURAHA NA NDEREMO, WAKATI BWANA MBURUJA MMBATA NA IRENE MNGAZIJA WALIPOFUNGA NDOA APRILI 18, MWAKA HUU JIJINI TANGA NA KUFUATIA SHEREHE YA KUWAPONGEZA.







# MITINDO



# JISTIRI NA HIJAB

KWA wanawake waumini wa Kiislamu katika kipindi hiki cha mwezi wa ramadhani, vazi la Hijab limekuwa muhimu katika kutengekeza nguzo hiyo ya kiimani.

Vazi hili ambalo kiasili linatoka Uarabuni, limepata umaarufu kwa watu wa imani zote na imekuwa kawaida kuwaona wakiwa katika mtindo huo bila kikwazo chochote.

Hijab, ambalo ni kitambaa maalum kinachoficha kichwa na kubakisha uso pekee, leo imepata umaarufu hata miongoni mwa wawakilishi wa dini nyingine.

Wabunifu wanatengeneza vazi hili katika mitindo ya kisasa ikiwa na nakshi na rangi mbalimbali .

Hata hivyo, namna ya kufunga hijabu imekuwa kazi ngumu kwa wale wasiofahamu, lakini kwa wale waliokulia katika mazingira ya vazi hilo kwao ni jambo jepesi.

Jinsi ya kufunga hijab

Kuna njia nyingi za kufunga hijab. Kwanza kabisa, ni lazima ieleweke kwamba urefu na upana wa kitambaa ni lazima angalau kiwe na mita moja na nusu.

Ukubwa huo anapaswa kufunika kichwa chote na kifua, masikio, shingo na nywele.

Baada ya kukusanya nywele zote ni vizuri kuweka kitambaa juu ya paji la uso pamoja kuweka mpaka wa nywele.

Pia kuwe na umbo pembe tatu nyuma ya kichwa chini ya nywele, na kitambaa kifike chini ya kidevu.

UREMBO



# BAKI NA RANGI YAKO

KUBADILI rangi ya ngozi imekuwa kama jambo la kawaida miongoni mwa wanawake, wanachoamini kuwa na muonekano mweupe ni ishara ya rembo na utanashati.

Kubadili kutoka weusi wa asili kuwa weupe wa mzungu, ni mtindo ulioanza siku nyingi, lakini kila siku mbinu na matumizi ya dawa za kubadilisha ngozi zinabadilika.

Huko nyuma watu walitumia vipodozi vikali vyenye viambata hatari pamoja na mchanganyo wa vimiminika moto ambavyo huchubua ngozi ya juu na kuacha ile ya kati ambayo ina rangi nyeupe.

Lakini kutokana na mabadiliko ya teknolojia, baadhi ya wanawake wanatumia njia ya kisasa ya kufanya upasuaji au kupandikizwa kemikali ambayo hubadilisha rangi taratibu.

Mastaa kadhaa hapa nchini, Marekani, Uingereza na Afrika ya Mashariki. wamekuwa wakifanya kila wawezalo ili kupata dawa hizo.

Hata hivyo, njia zote zimeelezwa zina athari nyingi kwa binadamu, kwani uzuri wa ngozi unakuwa wa muda mfupi na badala yake muda mwingi unakuwa wa shida na mashaka.

Miongoni mwa kemikali maarufu ambayo huchanganywa ndani ya vipodozi hivyo kwa lengo la kubadili Rangi ya ngozi ni "hydroquinone".

HYDROQUINONE INAVYOBADILI NGOZI.

Katika ngozi ya mwanadamu kuna chembechembe ambazo huitwa Melanin ambayo kazi yake ni kuipa rangi ngozi na kuilinda kutokana ni miale ya jua yenye madhara.

Kemikali ya Hydroquinone inakwenda kuzuia utengenezaji wa melanin kwenye mwili wako hivyo ngozi hupoteza Rangi yake ya asili na ulinzi.

Tafiti ya kisayansi zimethibitisha madhara mbalimbali yanaweza kujitokeza ikiwamo saratani ya ngozi.

Pia mtu anapata magonjwa ya ngozi kama kuwashwa, kuvimba, kutokwa mabaka na kupata mzio.

Pia kutokana na ngozi kutokuwa na ulinzi, mtu anapata matatizo ya kupumua pamoja na kuunguzwa na jua isivyo kawaida.

Athari nyingine ni mtu husika mwili wake kuzalisha chembechembe za rangi tofauti na kusababisha kuwa ra rangi mbili au zaidi kwenye ngozi.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# VIPAPATIO VYA KUOKA

**Mahitaji**

VIPAPATIO vya kuku kilo moja, yai moja, kikombe cha unga wa ngano na kikombe kimoja cha siagi.

Pia weka vijiko vitatu vikubwa vya soya sauce,vijiko vitatu vya maji safi na salama na kikombe kimoja cha sukari.

Mahitaji mengine ni robo kikombe cha vinegar, robo kijiko cha unga wa kitunguu saumu, kijiko 1 kidogo cha chumvi

**Maelekezo**

Hizi 'chicken wings' zinachovywa kwenye mayai kisha kukaangwa kwa muda mfupi kwenye siagi. Baada ya kukaanga vinachovywa kwenye sauce na kisha kuokwa. Zikiiva utapata ladha tamu ya chicken wings laini na tamu.

**JINSI YA KUOKA**

Washa oveni kwenye nyuzijoto 350, kata vipapatio vya kuku katikati, chovya kwenye mayai na kisha chovya kwenye unga. Hakikisha mayai na unga vimeenea vizuri.

Bandika chombo jikoni kwenye moto wa wastani, acha kipate moto kisha weka siagi. Acha iyeyuke na kisha weka vipapatio ya kuku na kanga hadi vibadilike rangi.

Kwenye bakuli ya wastani, changanya soya sauce, maji, sukari, vinegar, kitunguu saumu, na chumvi. Koroga vizuri hadi mchanganyiko uwe sawia. Nyunyizia sauce juu ya vipapatio vya kuku.

Weka tena vipapatio kwenye oveni, oka kwa muda wa dakika 30 to 45, halafu nyunyiza 'sosi' juu ya vipapatio mara kwa mara. Vikiiva epua na weka pembeni ni tayari kwa kuliwa

***(Kwa msaada wa Misosi Blog)***



# MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

## UMUHIMU WA MALIGHAFI BORA KATIKA UJENZI NYUMBA IMARA



LEO katika nyumba tutaangalia namna ya kuzingatia kupata malighafi bora wakati wa ujenzi kwenye nyumba ili kuepuka matatizo yanayoweza kutokea baadaye ikiwamo fangasi.

Katika kuepukana na tatizo la fangasi kwenye nyumba linalosababishwa na kutumia malighafi zisizo na ubora, nilizungumza na mtaalam wa masuala ya ujenzi, Joseph Nyamihonga.

Yeye anasema ni muhimu sana kuzingatia ubora wa malighafi zote zinazotumika katika ujenzi wa nyumba kwa sababu bila kufanya hivyo mbele huwa kuna majuto.

Anatolea mfano kwamba karatasi ngumu za plastiki, matofali, nondo, milango, madirisha na malighafi zote zinapaswa kuhojiwa ubora wake kabla hujazitumia.

"Malighafi dhaifu haziwezi kuhimili changamoto za mazingira yenye unyevunyevu kwa muda mrefu, ni hasara na kadhia kwa nyumba hata kama haupo kwenye maeneo ya majimaji utaratibu wa ubora upo palepale, mvua za upepo hulowanisha ukuta kwa nje na kukuletea madhara hadi ndani hasa kubanduka kwa rangi."

"Katika kutafuta malighafi ni bora kuepuka propaganda za masoko huria za vifaa vya ujenzi ukashindwa kuhoji ubora na matumizi sahihi kwa chochote unachonunua kwa sababu unatoa pesa na sio mawe," anasema Nyamihonga.

Anasema jambo lingine linalochangia fangasi kwenye nyumba ni kutozingatia utaalamu wakati wa ujenzi.

"Mara nyingi huwa nawakumbusha sana wale wanaojenga nyumba zao ninapokutana nao, kwamba ni lazima kujiridhisha na ubora wa fundi wako, kabla hujampa kazi ya ujenzi kwenye nyumba yako lazima uhakikishe mafundi wako wanatandika karatasi ngumu ya plastiki kwenye msingi wa nyumba, msingi usiwe chini sana kutoka usawa wa ardhi, kuhakikisha 'gata' zinafungwa vizuri kuepuka kuvujisha maji kwenye kuta, watumie saruji na si rangi."

"Kuhakikisha wanatumia niru na gypsum' kwenye maeneo yenye matumizi ya maji, matumizi sahihi ya rangi kwenye kuta na sakafu, na kuepuka mzunguko mkubwa wa mabomba ya maji safi na maji taka, kuweka nyumba iwe upande wenye mwinuko, na mashimo ya maji taka au visima yawekwe pembeni upande wa chini na kama umejenga paa lenye zege hakikisha unafanya usafi mara kwa mara na kutoruhusu kuhifadhi maji hata kama umeweka malighafi zisizopitisha maji hayo."

Anashauri kwamba ujenzi unahitaji umakini na usimamizi wa hali ya juu sana kuhakikisha ubora unazingatiwa kwenye kila hatua.

Kwamba ni rahisi kupambana na mazingira yenye majimaji kwenye ardhi wakati wa ujenzi kuliko kuzuia baada ya ujenzi kwa sababu ni gharama na inahitaji marekebisho kila baada ya miaka michache kutokana na aina ya malighafi zilizotumika.





# MPANGILIO

## JINSI YA KUCHAGUA MAPAZIA

KUNA aina nyingi za mapazia ambayo unaweza kuweka katika nyumba yako na ikapendeza. Lakini leo nitakupatia dondoo ya kuchagua aina ya mapazia ambayo yataifanya nyumba yako kubadilika na kuonekana ya kisasa zaidi.

**Aina ya Kifaransa**

Mapazia haya yanajulikana kutokana na kuwa na michoro mikubwa, na ina idadi kubwa ya urembo. Haya ni mapazia mazuri sana kwa chumba cha kulala.

**Aina ya Kiaustria**


Kwa kawaida inakuwa na pembe nyingi zilizo sawa inayofanana na ile ya Ufaransa, lakini ina urefu wa wastani. Aina hii ya mapazia yanaweza kuwekwa katika chumba kikubwa na kuonekana kama cha watu matajiri.

**Mapazia ya Kingereza**

Mapazia haya yanakuwa marefu na yenye mapambo mengi yanayoounganisha pande zote. Juu ya kitambaa lazima iwe na bendi za wima. Mfano huu wa mapazia ya chumba cha kulala huleta muonekano wa kimahaba zaidi. Unaweza kuweka ya rangi yoyote.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
WATANI SPESHO
HIVI NANI HUYO WATU TUSOMA RAMANI YA AFRIKA KUELEKEA UBINGWA!
EMBU TOKA NA 'BUNGO LIMAO NA UKWAJU ILI TUONE UMAHIRI WAKE
POOOOOOOOOOOOOOO!!!
DABI NI VITA YA MUDA HUO HUO IKIMALIZIKA TU KAZI IENDELEE...
NDIO NAIWAZIA KAZI YA "KAWIZA CHIPSI" KAMA NIKAFANYE KUFURU AU NIKAWAPAPASE KAWAIDA
NADHIHIRISHA KUWA MATOKEO 'NILIYATARAJIA' ACHA NIWA-KERE...
UTANI WA KIBWEGEBWEGE MPAKA TUNAFOJI MARADHI KUEPUKA MAUDHI!
KAMEZA VIDONGE VYA PRESHA ASI-BUGHUDHIWE
ZZ!
ZZ!
PALE KWA MKAPA NIMESHUHUDIA SAFARI YA MNYAMA KWENDA KULETA NDOO YA UBINGWA WA AFRIKA...
NITATEMBEA BILA NGUO NITAZUNGUKA MJI MZIMA
KWA FURAHA AU UCHIZI?
HUO NI WEHU!
HAWA NDIO WANGA WENYEWE
KAMA VIPI APIGWE CHINI
"EH!
KAKA UMELALA NA VIATU!
KWANI SINA MKE KAMA WEWE?
NIMETAMBA SANA, SASA NITAWAEPUKAJE NILIOWATAMBIA WAKATI NAWADAI NIMEITWA NILIPWE?
ZIMA SIM! LALA
TUFANYE UTANI WOTE! LAKINI SITANI UTANI NA MKE WANGU
KUMBE HUTANIANI NAE NDIO MAANA ANAPENDA TUTANIANE!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
MUUNGWANA AKIVULIWA NGUO?..........

HABARI KIMATAIFA

## Mahama kuwa mpatanishi Somalia

**Adis Ababa,** ETHIOPIA

UMOJA wa Afrika (UA) umemchagua Rais wa zamani wa Ghana, John Mahama, kuwa mpatanishi maalum wa Somalia katika kusaidia kutatua mgogoro wa kisiasa.

Kulingana na taarifa ya umoja huo, jukumu la Mahama mwenye miaka 62, litakuwa kutafuta suluhisho la pamoja ili uchaguzi wa nchi hiyo uliokwama uweze kufanyika ndani ya muda mfupi ujao.

Kiongozi huyo, alitarajiwa kusafiri kuelekea Somalia hivi karibuni.

Mwenyekiti wa Halmashauri Kuu ya Umoja huo, Moussa Faki, aliwahimiza viongozi wa Somalia kuingia katika majadiliano kwa nia njema ili kupata suluhu ya pamoja katika mgogoro huo.

Faki alisema nchi hiyo inahitaji serikali iliyochaguliwa kidemokrasia iliyo na uhalali na mamlaka ya kusuluhisha changamoto nyingine za kisiasa na kikatiba zinazotishia uthabiti wa taifa hilo.

**DW.**

## Serikali ya Ethiopia yalaumiwa

**Adis Ababa DIS,** ETHIOPIA

KIONGOZI wa kanisa la madhehebu ya Orthodox nchini Ethiopia, Abune Mathias, ameituhumu serikali kwa kutaka kuliharibu eneo la Kaskazini mwa Tigray.

Katika matamshi yake ya kwanza kuhusu vita katika eneo hilo, Abune alisema vikosi vya serikali vinafanya kazi usiku na mchana kuuharibu mji huo.

Pia alilalamikia mauaji yanayoendelea eneo hilo yana nia ya kuwaondoa kabisa watu wa kabila la Tigray katika nchi hiyo. Taarifa kutoka kwa kiongozi huyo ambayo ilitolewa kupitia mkanda wa video, inawakilisha ukosoaji wa nadra kutoka kwa kiongozi wa juu wa kidini kuhusu mzozo katika eneo la Tigray, uliodumu kwa miezi sita.

Vikosi vya serikali ya Waziri Mkuu Abiy Ahmed, viliwaondoa wapiganaji wa chama cha TPLF, baada ya kutuhumiwa kufanya mashambulizi dhidi ya wanajeshi wake.

**DW.**



Polisi wa Israel wakikabiliana na muumini wa Kipalestina wakati ilipotokea vurugu katika msikiti wa Al Aqsa mjini Jerusalem juzi. Zaidi ya watu 200 walijeruhiwa katika tukio hilo. **(PICHA: AFP)**

# Watu 200 wajeruhiwa kwenye ghasia Jerusalem

**Jerusalem,** ISRAEL

ZAIDI ya watu 200 wamejeruhiwa usiku wa kuamkia jana wakati ilipoibuka ghasia kati ya Wapalestina na polisi wa Israel katika eneo la msikiti wa Al-Aqsa mjini Jerusalem.

Katika idadi hiyo, Wapalestina 194 wamejeruhiwa na polisi sita wa Israel nao wamepata majeraha. Tukio hilo lilitokea katika maeneo ya msikiti wa Al-Aqsa na mitaa ya mashariki mwa Jerusalem. Polisi wa Israel walitumia risasi za mipira kukabiliana na waumini wa kiislam wa Kipalestina waliokuwa wakirusha mawe, chupa na fataki.

Katika kukabiliana na hali hiyo, polisi pia walilifunga lango la kuelekea msikiti wa Al-Aqsa ndani ya mji wa zamani huko Jerusalem.

Maelfu ya waumini wa Kiislamu walikuwa wamekusanyika kwa ajili ya swala ya ijumaa ya mwisho ya mwezi mtukufu wa Ramadhani. Mvutano uliongezeka baada ya polisi wa Israel kuimarisha ulinzi mkali katika eneo la msikiti.

Tangu kuanza kwa mfungo wa Ramadhani, na kucheleweshwa kwa uchaguzi wa bunge wa palestina, machafuko yameibuka katika Ukingo wa Magharibi na Mashariki mwa Jerusalem.

Ghasia zimeongezeka katika wiki za hivi karibuni baada ya Waplestina kupinga vizuizi vya Israel kuyafikia maeneo ya mji wa zamani wakati wa mfungo wa mwezi wa Ramadhan, na pia kuongezeka kwa hasira inayotokana na uwezekano wa familia za Kipalestina kuondolewa kwenye makazi yao katika eneo la Sheikh Jarrah kupisha ujenzi wa makazi ya wayahudi.

Marekani imetoa wito kupunguza mivutano na kusema kitisho cha kuwaondoa watu kwenye makazi yao, kitaathiri zaidi hali katika eneo la Mashariki mwa Jerusalem, wakati Umoja wa Mataifa nao ukionya kwamba kuwaondoa watu kinguvu kunaweza kuhesabiwa kama uhalifu wa kivita. Ghasia hizo zimetokea katika siku ya Al-Quds ambayo huadhimishwa kila mwaka kuonyesha mshikamano na Wapalestina. Maandamano ya kuadhimisha siku hiyo yalifanyika nchi tofauti zenye idadi kubwa ya Waislamu. Kiongozi wa juu wa Iran Ayatollah Ali Khamenei, alisema israel ni nchi inayochochea ugaidi.

Mahakama ya juu ya Israel itatoa uamuzi juu ya kuondolewa Wapalestina eneo la Sheikh Jarrah siku ya kesho, siku hiyo itagongana na maadhimisho ya kila mwaka ya Israel kudhibiti Jerusalem Mashariki baada ya vita ya Mashariki ya kati ya mwaka 1967.

**DW**

# India yazidi kuelemewa wagonjwa wa corona

**Mombay,** INDIA

MAJIMBO mawili ya kusini mwa India yameungana na mengine kuweka masharti ya kutotoka nje, wakati visa vya maambukizi ya corona vikipanda maradufu.

Serikali ya Waziri Mkuu Narendra Modi, inaendelea kupata shinikizo la kuweka vizuizi vya kitaifa kukabiliana na janga hilo.

Mji ulioathirika zaidi ni Bengaluru katika jimbo la Karnataka, ambao una zaidi ya watu laki tatu walioambukizwa.

Hata hivyo, wataalamu walisema hali huenda ikazidi kuwa mbaya kufuatia mji wa tatu kwa ukubwa nchini India, kukumbwa na uhaba wa gesi ya Oksijeni, pia hospitali zimejaa wagonjwa na pia maeneo ya kuchomea maiti yamezidiwa. Masharti ya kutotoka nje pia yametangazwa katika Jimbo la Tamil Nadu, baada ya zaidi ya watu 26,000 kuambukizwa virusi vya corona juzi Ijumaa pekee.

Makali ya ugonjwa huo yalianza kuonekana mwezi wa Februari, wataalamu wanasema hali hiyo imechangiwa na hatua ya serikali kukubali mkusanyiko wa watu katika sherehe za kidini na mikutano ya kisiasa.

India ina idadi Jumla ya watu milioni 21.8 walioambukizwa virusi vya corona na vifo zaidi ya 240,000.

**DW**

MAKALA

# MADHARA YA KUJICHUBUA



Na Magabilo Masambu

KUJIKUBALI ni hali ya kuridhika na jinsi ulivyoumbwa na Mwenyezi Mungu. Katika imani mbalimbali za dini, tunaamini na kufundishwa kwamba kila alichokiumba Mwenyezi Mungu ni chema, japo imani hii kwa muda mrefu sasa inaendelea kutoweka miongoni mwa wanadamu.

Hali hiyo inatoweka kutokana na baadhi ya watu kudhani kwamba walivyoumbwa walikosewa, hivyo wanahitaji kumrekebisha Mungu katika kazi yake ya uumbaji.

Ni wazi kuwa hata kama Mungu angelikuwa na upumbavu wa kiwango cha chini zaidi basi upumbavu huo bado ungelikuwa zaidi ya hekima alizo nazo mwanadamu. Hata kama Mungu angelikuwa na udhaifu wa kiwango cha chini zaidi, bado udhaifu huo ungelikuwa imara zaidi kuliko uimara alio nao mwanadamu. Maana yake ni kwamba kwa vyovyote vile, hakuna namna ambayo mwanadamu atakosoa au kurekebisha kazi ya Mungu aliyokwisha kuifanya katika uumbaji wake.

Nayaandika haya kwa sababu kumezuka tabia ambazo naziona ni tabia mbaya kabisa kimaadili, kiimani, kiafya, kijamii na kiuchumi na zimeendelea kusambaa na kuimarika siku hadi siku. Tusipojirekebisha tutapoteza nguvu kazi ya taifa na utaifa wetu kama Watanzania na Waafrika kwa ujumla.

Leo tuzungumze kuhusu tabia ya watu kujichubua (mkorogo kwa baadhi wanawake na wanaume). Tabia hii ilianza kujitokeza zaidi miaka ya 1980 katika maeneo ya watu wenye ngozi nyeusi. Jambo hili liliendelea kupata umaarufu mpaka leo watu wameona kwamba ni utamaduni mzuri sana. Hapa nitaeleza madhara yake kwa uchache tu ili wale wote wenye tabia hii wajitafakari na ikiwezekana waachane na utamaduni huu.

Moja kiafya, kansa ya ngozi. Mtu anapojichubua anatumia njia mbalimbali za kutumia dawa au kemikali. Wako wanaomeza vidonge, kujidunga sindano, wanaopaka mwilini. Njia zote hizi zina madhara katika ngozi ama mwilini kwa ujumla. Wasichofahamu ni kwamba katika ngozi ya binadamu kuna kitu kinaitwa melanini ambayo kazi yake ni kuipa ngozi rangi.

Kubwa zaidi, melanini hii inalinda ngozi dhidi ya mionzi ya jua (infrared) ambayo ikiondolewa itasababisha mionzi ya jua kupiga moja kwa moja kwenye ngozi ya ndani na kusababisha mafuta ya mwili kuchomwa na matokeo yake kutengeneza vidonda ambavyo vinatengeneza kansa, kwa sababu ngozi itakuwa haina uwezo wa kujilinda dhidi ya maambukizi yoyote.

Pili, kiuchumi. Mtumiaji anapoanza itamlazimu kuendelea kuzitumia dawa hizo ambazo ni gharama kubwa na pale anapoziacha rangi ya ngozi yake inakuwa na rangi zenye mabaka, kitu ambacho akitamfanya aonekane kama alivyokusudia. Kwa hiyo ili awe na mwonekano anaouhitaji, atalazimika kuwa mtumiaji wa kudumu, hivyo kutumia fedha nyingi zaidi katika kutengeneza ngozi. Wakati mwingine itamlazimu kupata kansa ya ngozi na kuhitaji fedha nyingi zaidi kuanza kujitibia, ambayo pia inaweza kusababisha umauti.

Kutweza utu, mtu anapojichubua anaudhalilisha utu wake kwa kutojikubali na kutaka kufanana na wazungu, kitu ambacho ni aibu kubwa. Waafrika tunadhalilisha utu wetu si kwamba nawachukia wazungu hapana lakini kwanini tusijikubali kama Mungu alivyotuumba?

Nani na ni lini utafiti umeonyesha kuwa mtu akiwa mweupe ndiyo anatakuwa na mwonekano mzuri? Ni nani anayesema ili uwe mzuri sharti uwe mweupe kwani weusi hatupendezi? Waafrika weusi ni lazima tulinde heshima na utu wetu bahati mbaya tu hatujatambua thamani ya ngozi yetu.

Tulipowapinga wakoloni hatukumaanisha kisiasa na kiuchumi pekee bali hata kijamii. Tunapotamani kuwa wazungu wakati sisi ni waafrika tunajifedhehesha. Tukatae utumwa, tujithamini kwa sababu tumeumbwa kwa mfano wa Mungu. Hatuna sababu ya kujidhalilisha kiasi hiki.

Nakubali kwamba dunia imekuwa kijiji na kwamba huu ndiyo ukisasa, lakini haimaanishi kila kitu tuige, mbona wao hawajipaki rangi nyeusi ili tufanane nao? Tunapaswa kuiga yenye manufaa kutoka kwao lakini hatupaswi kuiga kila jambo.

Nne, kiimani, kama nilivyotangulia kueleza hapo mwanzo unapojichubua unajaribu kupeleka ujumbe kwa muumba wako kwamba, hukupaswa kuwa hivyo unavyoonekana na kwamba ulipaswa kuwa kama mzungu, kitu ambacho nadhani kwa imani zote ni chukizo kwa Mungu.

Lazima tutambue kwamba, tulishapewa thamani kubwa sana mbele ya Mwenyezi Mungu. Hatuhitaji kupewa thamani yoyote na wanadamu kwa kuwa wanaouza kemikali hizo, ndio hao hao wanaouza dawa za kansa. Kwa hiyo wanatengeneza pesa nyingi sana kwa kutumia udhaifu wetu wa kutojikubali jinsi tulivyo.

Tano, kisaikolojia. Wale wanaojichubua wakapata madhara hasa ya ngozi. Huwa wanapata wakati mgumu sana kukaa kwenye makundi ya watu wengine kutokana na walivyoharibika. Mara zote hukosa raha kutokana na kufikiria jinsi watu wengine wanavyowatazama na kuwachukulia, hivyo wengine wanalazimika nyakati zote kujifunika gubigubi ili kuficha aibu ya mwonekano wao. Kwahiyo kisaikolojia wanakuwa hawako sawa.

Baadhi vijana wa kiume nao hawako mbali. Hii ni hatari sana kwa taifa ambalo uchumi wake kwa asilimia kubwa tunategemea kilimo kama shughuli kuu ya uzalishaji, tutalima kweli? Taifa litakuwa na nguvu kazi kweli? Tunakusudia kutengeneza taifa la watu wa aina gani? Kila mmoja wetu anapaswa kujiuliza maswali haya.

Ushauri wangu kwa serikali, mambo haya tusiyaonee aibu hata kama wanaofanya ni wake au waume zetu, ndugu zetu tuyakemee waziwazi kwa kuwaelimisha juu ya madhara yatokanayo na tabia hii.

Tukiyaonea haya leo kesho hatutakuwa na taifa la watu wenye afya bora. Natambua juhudi za serikali katika kuthibiti uingiaji wa kemikali hizo, lakini ni ajabu tu kwamba hata wenye dhamana ya kuzuia nao baadhi yao ni watumiaji. Kwa hiyo serikali ikidhamilia katika jambo hili, naamini wananchi wataunga mkono vinginevyo tutakuwa na taifa la watu ambao hawatakuwa wanajiamini kwa kila jambo kwa sababu watakuwa hawajikubali.

**Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania. 0689157789**

**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Enzi za unga wa Yanga, maduka ya kaya*



Na Adam Fungamwango

SIKU moja nilikuwa nazungumza na baba yangu maongezi ya kawaida tu. Akaniambia enzi zetu sisi chai inapikwa nyumbani halafu unatumwa sukari dukani. Na dakika mbili unarudi kutoka dukani unampa mama sukari na chai inanyweka.

Mimi kacheka. Akauliza unacheka nini. Nikamjibu ya kweli hayo baba? Naye akaniambia kuwa huwezi kuamini kwa sababu ninyi watoto wa sasa mmeanza kupata akili kipindi hiki ambacho bidhaa adimu. Hakuna sukari, unga, mchele wala sabuni madukani. Hiyo ilikuwa mwanzoni mwa miaka ya 1980 hadi katikati.

Miaka mingi baadaye, mwishoni mwa miaka ya 1980 hadi miaka ya 1990 ndiyo nilianza kumwelewa na kumuamini mzee nini alichokuwa akiongea.

Ni kwamba bidhaa zilianza kuonekana madukani na ilikuwa ni kweli sasa kinamama walikuwa wanatutuma sukari dukani wakati chai imeinjikwa. Mwanzoni ilikuwa ni kama miujiza hivi, lakini baadaye ikazoeleka.

Kwa sasa kuna baadhi ya vijana wanaona kama vile nchi ina matatizo ya uchumi, lakini wangeuwauliza wakubwa wao wangewaambia kilichotokea mara baada ya kumalizika kwa Vita vya Kagera. Na wangewaambia watoto wa vijana wao kuwa kulinganisha na kipindi kile cha mpito, hivi sasa wananchi wa Tanzania wanaishi maisha ya raha sana.

Ni pesa yako tu. Kipindi kile hata ukiwa na pesa unaweza kulala njaa na hasa mijini, hususan Dar es Salaam. Angalau hata vijijini ungeweza kupata walau mihogo, mahindi, ndizi na vyakula vingine.

Vita vya Kagera vilipiganwa kati ya Tanzania kuanzia Oktoba 30, 1978 hadi Aprili 11, 1979, kugombea Mkoa wa Kagera ambao Rais wa Uganda wakati huo, Idi Amin Dada, alidai Mto Kagera na baadhi ya ardhi ya mkoa huo ni mali yake.

Tanzania iliibuka kidedea kwenye vita hivyo kwa kuichakaza Uganda. Hata hivyo, vita ni vita. viliacha makovu pamoja na uchumi kuyumba, kiasi cha wabongo kutangaziwa 'kufunga mikanda'.

Hali ya chakula ikaanza kuwa mbaya kiasi cha kupata msaada wa unga na mahindi kutoka nchini Marekani ambao kwa kiasi kikubwa uliwasukuma Watanzania na kutibu njaa, hadi hali iliporejea kwenye hali yake ya kawaida miaka kadhaa baadaye.

Unga huo si kama huu ambao tunaouna hivi sasa mweupe. Ulikuwa wa rangi ya njano. Na hata mahindi yake yalikuwa na rangi hiyo. Ukipika ugali unakuwa wa rangi ya njano. Wabongo wakaupachika jina, wakauita 'unga wa yanga'. Unga huo ukawa maarufu sana kiasi kwamba hakuna aliyekuwa mtoto, kijana au mzee wa kati huo ambaye leo yupo hai akakosa kukumbuka hali hiyo.

Mbali na uhaba wa chakula. Kulikuwa pia na uhaba wa mahitaji mengine kama sabuni, dawa za meno, miswaki na vitu vingine vingi ambavyo nitakuja kuvielezea siku kwenye safu hii.

Ukawekwa utaratibu ili wananchi wote wapate. Unga huo ukawa haupelekwi kwenye maduka ya kawaida ya watu binafsi. Yakaundwa maduka ya ushirika. Kila wananchi wa eneo fulani walikuwa wakijiorodhesha majina chini ya viongozi wao ambao ni wajumbe wa nyumba kumi na kufungua duka. Haya ndiyo yaliyokuwa yakiitwa maduka ya kaya. Nia ilikuwa nzuri, lakini tatizo utelekezaji wake ukawa mbovu kiasi yakafa kifo cha asili.

Kila mtu anaandikisha kama ana mke na idadi ya watoto alio nao. Wenye watoto wengi walipata kilo nyingi za unga kuliko wenye watoto wachache. Unga pamoja na bidhaa zingine kama mchele au sukari, mafuta ya taa, siku vikija, vinauzwa kwa kufuata reja iliyopo.

Kama ulipata wiki hii, basi mpaka wiki ijayo. Ukimaliza chakula chako mapema utajua mwenyewe. Rushwa kama kawaida ilikuwapo. Wauzaji pamoja na wajumbe wa nyumba kumi hawakuwapatia wanakaya mahitaji yao wakati mwingine kwa kuwarusha hata wiki tatu, huku unga, mchele au sukari wakiwauzia watu wengine kwa kiasi kikubwa cha pesa, kilichoitwa mwendo wa kuruka.

Hali hii wakati mwingine ilisababisha mzozo mkubwa. Kali kuliko yote wakati mwingine wanakaya wanalazimishwa, ukinunua unga, mchele au sukari ni lazima ununue na maharagwe, kibiriti, au kunde. Yaani ni lazima ununue na bidhaa ambayo wao wanaona haiuziki kwa urahisi au haina wateja wengi. Hayo maharagwe yaliyokuwa yanauzwa kwa lazima ni yale ambayo hayakuwa yanaiva kwa urahisi. Wakati mwingine ni lazima yatiwe magadi.

Wakati huo huo kulikuwa na magari yaliyokuwa yakisambaza chakula, kama unga, mchele, sukari yaliyoitwa Magari ya Ugawaji, siku yakipeleka kwenye maduka binafsi ambapo inakuwa ni kwa nadra sana, foleni yake inakuwa si ya kawaida. Kuna watu wanaweka mawe, makopo kama foleni kuanzia alfajiri. Wakati mwingine kunakuwa na ugomvi, patashika nguo kuchanika ili mradi tu kila mmoja anataka yeye awe wa kwanza kupata.

Magari ya Ugawaji yakionekana tu, basi watu wanayafukuza ili kuona wataishia duka gani. Watu waliwahi kufukuza hadi gari la maiti wakidhani ni la ugawaji.

Haya ni matukio yaliyotokea huko nyuma hapa nchini ambayo hayatafutika na kubaki kama kumbukumbu kwa vizazi vingi vijavyo kuona Tanzania ilipokuwa wakati mwingine inapitia vipindi vigumu.


Kizazi ambacho kilikutana na hali hiyo ambacho bado kipo, waliangalia na hali ya sasa, pamoja na kusikitika, wakikutana na kusimualia vimbangwa walivyokuwa wanakutana navyo, wanaichukulia hali jinsi ilivyokuwa ni kama burudani iliyotikisa.

# HADITHI

# Sumu ya Mapenzi-5

KWANI mapenzi ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka wewe? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana? Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa.

Donald, Kijana msomi aliyetoka nchini Marekani, anarejea nchini Tanzania. Anakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake. Lakini pia anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Usikose hata nakala moja ya riwaya hii tamu na ya kusisimua.



**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**

"Vipi mbona kama huna furaha na mimi?"

"Nimekwambia naumwa wewe nenda kwenu, leo sijisikii vizuri."

"Kama hujisikii vizuri mimi nipo hapa kwa ajili ya kukuliwaza."

"Nimekwambia sitaki kuliwazwa. Mtu analiwazwa akiwa amechoka, siyo kuumwa, unasikia Doris."

"Basi naondoka."

"Nenda."

Zilikuwa sauti za wapenzi wawili. Donald na Doris. Doris alikuwa amepigiwa simu na mama Donald, Eva. Mama ambaye alichangia sana kupatikana kwa Doris, msichana mrembo na msomi ili awe mkwewe alimwita baada ya kijana wake kusema kuwa ni mgonjwa.

"Mwenzako leo hajisikii vizuri, sasa yuko peke yake, njoo umuangalie kidogo, nadhani anaweza kuwa sawa kidogo akikuona."

Doris alikmbuka taarifa aliyopewa na mkwewe mtarajiwa.

"Mama Donald kanifukuza. Alisema huku akiangua kilio."

"Kwa nini?"

"Sijui, kaniambia niondoke."

"Hivi huyu mwana ana wazimu? We Donald kwa nini unamfukuza mwenzako?"

"Yeye mwenyewe ndiye aliyeniuliza niondoke? Mimi nikamwambia ondoka, Sasa hilo ni kosa?"

Doris, msichana mrembo na msomi anayetoka kwenye familia ya kitajiri, pamoja na kuhitajiwa na wanaume wengi wenye nyadhifa mbalimbali na wafanyabiashara wakubwa, alitokea kumpenda Donald kijana mnatashati ambaye naye ametoka kwenye familia ya kitajiri.

Kijana anaonekana kama haelewekі na hana msimamo. Hakumchagua Doris, ila ameletewa na wazazi wake kwa sababu ya kumlinda na kumfanya awe na utulivu na moyo kwa sababu tayari wameshamkabidhi kuendesha kampuni yao.

"Mama mimi naumwa. Yeye aende tu, nikishapona aje. Mimi nataka niwe peke yangu hasa wakati huu siku sawa. Huwa napenda nikiumwa niwe peke yangu kwanza."

"Sasa ukimuoa itakuwaje?"

"Hapo sasa nitakuwa nimeshaoa, lakini kwa sasa aniache kwanza. Kesho nikipona nitakupigia uje." Donald alimwambia Doris ambaye alionekana kujisikia vibaya. Hakuzoea kuambiwa hivyo na mwanamume yeyote. Hakuna mwanamume ambaye anaweza kumwambia mwanamke kama Doris nenda. Hata hivyo, Doris alivumilia kutokana na kumpenda mno Donald.

**************************

Sadiki alimkaribisha Donald nyumbani kwake kwa mara ya pili. Mara ya kwanza ilikuwa kuja kumwona rafiki yake kwa sababu alikuwa hajaonana naye miaka mingi.

**"Usijali, kuna siku nitakwambia mapema kuwa nakuja, na kukuachia masaa ya kujipamba kama malkia." Baada ya kumaliza maneno hayo vicheko vilizidi.**

Safari hii aliamua kuja tu kumtembelea.

"Yaani Donald sikuelewi. Leo umenipigia simu ghafla tu kuniambia uko njiani unakuja, halafu huyu hapa, vipi?"

"Tulia kwanza tutaongea."

Sadiki alicheka. halafu akasema "Au tayari watoto wa uswazi washakuchangana?"

Donald ilikuwa bado kidogo aangue kicheko. Lakini alisita. Hakutaka kumuonyesha rafiki yake kuwa yuko karibu na ukweli.

Ilikuwa baada ya dakika tano tu, ndipo Donald alipomwambia Sadiki ampigie simu Tausi kuwa yuko kwake.

"Kwani wewe ulishindwa kumpigia au kumwambia kuwa unakuja?"

"Hapana. Ila wiki iliyopita tuliongea. likuwa anataka nimuongezee pesa ya matibabu. sasa nimekuja kumuangalia kama amepona. Na sikutaka kumwambia. Nilitaka nimshtukize tu kuwa nipo hapa."

"We Tausi njoo hapa nyumbani kwangu."

"Kuna nini wewe kama Sadiki?"

"Utakuja kuona huku huku."

"Mhh, we nawe kwa vituko. Haya nakuja. Na uniitie jambo la maana."

"Hakai mbali?" Donald aliuliza.

"Mtaa wa pili hapo. Muda si mrefu utamuona. Ndiyo atakuwa shemeji nini?"

"We nawe Sadiki acha mambo yako. Mimi nimeshakwambia ni 'mgonjwa wangu', nimekuja kumuona."

"Siku ile alipigika kweli kweli, kukosa wewe sijui ingekuwaje. Na sijui kama angepata pesa ya kwenda kujibia. Labda ndugu zake wangechangishana."

Dakika kumi baadaye walisikia hodi. Ilipigwa kwa kugongwa mlango na maneno pia.

Wala hala haikuihitaji kitu chochote kujua kuwa ilikuwa ni sauti ya Tausi. Hata Donald alishaanza kuifahamu kwa mbali.

"Karibu pia mlango uko wazi."

Tausi aliingia. Awali alionekana kama kuna kitu alitaka kusema, lakini ghafla alikuwa mpole.

Hakutegemea kuuona ugeni ule pale muda ule. Alivaa kijora na viatu vya kawaida tu. Nywele zake alisuka mabutu.

Alishindwa kusema chochote. Donald naye alishindwa kumkaribisha.

"Karibu." Sadiki alisaidia. Tausi alibaki amesimama. Hakujua akae au aendelee kusimama.

"Kaa hapo." Sadiki aliendelea kusimamia shoo ya watu ambao walikuwa hawaongei.

"Ka'Sadiki yaani umenikurupusha huko, sijaoga, sijabadilisha nguo, nilivyokuwa ndiyo hivi hivi jamani. Si ungeniambia ili angalau nikaoge tu jamani?"

"Si mimi Tausi. Aliyekuita ni huyu hapa. Mi mjumbe tu. Na siku zote Mjumbe hauawi."

"Samahani Tausi. Mimi ndiye niliyekwita." Donald alidakia.

"Na niliyemwita ni Tausi. Tausi kama yeye bila kujali yukoje na amevaa nini. Hata ungekuja umevaa gunia wala nisingejali." Alisema na kusababisha vicheko kutoka kwa wenzake.

"Usijali, kuna siku nitakwambia mapema kuwa nakuja, na kukuachia masaa ya kujipamba kama malkia." Baada ya kumaliza maneno hayo vicheko vilizidi.

"Ni hivi Tausi, mimi nimekuja kukuangalia tu mgonjwa wangu. Unaendeleaji?"

"Mimi nimeshapona. Nashukuru sana kwa msaada wako kusema kweli. Mimi sikutegemea hili. Nakushuru sana."

"Tuachane na hayo. Pesa zako za mchezo umeshalipwa?"

Ndipo Tausi alipokumbuka kuwa alishawahi kumwambia kuwa anadai pesa zake na mchezo ambazo ndizo zilikuwa amlipe dada aliyekuwa anapigana naye, Tatu.

"Nusu nimelipwa, zingine bado."

"Sasa kwa nini huwa mnacheza michezo ambayo hamlipani?"

"Kaka yangu we acha tu. Unajua sisi wanawake wakimwona mwenzao mnyonge ndiyo wanafanya hivyo. Wale wakorofi thubutu. Sisi ambao ukorofi wetu ni wa midomo tu tunadhulumiwa."

"Kifupi Tausi nahitaji au napenda kama utakuwa na nafasi, Jumapili ijayo kama hutojali nije kukuchukua pamoja na Sadiki. Nataka twende sehemu moja tulivu kusherehekea mimi na rafiki yangu Sadiki kukutana baada ya miaka mingi. Nimesoma naye huyu. Na nimekuchagua wewe kwa sababu ni kama nimeshaanza kukuzoea, tangu siku ile pale kwenye ugomvi."

Tausi hakupinga. Alijiona mwenye bahati kubwa. Akimwangalia kijana yule alionekana kama ni mtu makarimu, mcheshi na mwenye uwezo.

Hata alipoondoa Tausi hakulala usiku. Alimuwaza na kumuota pia. Akakumbuka pia alivyopewa kiasi cha shilingi laki tatu wakati wanaagana. Yeye ni mtoto wa kike. Aliziona dalili zote ya upendo kwake ndani ya kijana yule ambazo hajazidhihirisha wazi.

*Itaendelea Jumapili*



# ISHA MASHAUZI AKUMBUKA NDOA YAKE

MSANII wa muziki wa Taarab, Isha Mashauzi, amesema kitendo cha kuachwa na mume wake anakichukulia ni jambo lililopangwa na Mungu.

Amesema yeye na aliyekuwa mume wake, walikutana Visiwani Zanzibar na waliishi katika ndoa kwa mapenzi mazito.

"Nilifukuzwa nyumbani na mama baada ya kukutwa na rafiki yangu aliyekuwa amelewa, nikaenda kuishi Zanzibar, huko nilimpata baba mtoto wangu na baada ya hapo ndiyo ikabidi nirudi nyumbani tena kwa ajili ya ndoa, ingawa ndoa haikua riziki" ameeleza Isha Mashauzi.



# GIGY MONEY AENDELEA KUSOTA

JUHUDI za kumchomoa mwanamuziki wa kizazi kipya, Gigy Money, katika kifungo cha miezi sita zinaendelea kwa kasi, sasa barua nzito imepelekwa Baraza la sanaa Tanzania (BASATA) kuomba afunguliwe.

Katibu Mkuu wa Chama cha Muziki wa Kizazi Kipya, Samwel Mbwana 'Braton' amesema wamewaandikia BASATA kuhusu kuachiwa kwa msanii Gigy Money.

"Suala la Gigy Money lipo wazi na lipo mikononi mwa BASATA, tulishapeleka barua na tumewaomba pia tunategemea watalipatia ufumbuzi," amesema.

Januari 5, mwaka huu, Gigy Money alihukumiwa na BASATA kutojihusisha na masuala ya sanaa kwa muda wa miezi 6 na faini ya Sh. milioni moja kwa kosa la ukiukwaji wa maadili.

# Serikali yakubali yaishe

BAADA ya kuwapo na mvutano mkali kuhusu kanuni mpya inayoruhusu kuhakikiwa kazi za wasanii, Serikali imeamua kusitisha utekelezaji wa kanuni hiyo.

Uamuzi huo umetolewa jana na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, baada ya kukutana na wadau wa muziki nchini wakiwamo wasanii mkoani Dar es Salaam.

Awali Basata ilitoa agizo la kukagua nyimbo za wasanii kabla hazijapelekwa kwenye redio, televisheni na majukwaa mbalimbali.



## HABARI MICHEZO

# Arsenal wafikiria kumbakiza David Luiz

**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal inaripotiwa kuwa inafikiria kumsainisha mkataba mpya mlinzi wake, David Luiz.

Mkataba wa sasa wa nyota huyo mwenye umri wa miaka 34 kuendelea kuwapo hapo dimbani Emirates unafikia tamati Juni mwaka huu, huku uamuzi wa mwisho juu ya hatima ya nyota huyo ukitarajiwa kuwa utasubiri 2020/21.

Lakini kwa mujibu wa chanzo cha habari cha Brazil, Arsenal wanapima maamuzi yao ikiwa ni sahihi kumwongezea mkataba beki huyu kuendelea kuwapo hadi angalau Juni, 2022.

Hata hivyo, staa huyo pia amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa ikiwamo Benfica na Fenerbahce, wote wakiwa wanafuatilia kwa ukaribu mwenendo wa hatima ya mkataba wake.

Luiz amekuwa na kipindi kigumu akipata majeraha kadhaa msimu huu, lakini amecheza kwenye mechi 30 za michuano yote msimu huu chini ya Mikel Arteta, akifanikiwa kuona lango mara mbili.

Mlinzi huyo alishindwa kuwapo kwenye kikosi chake dhidi ya Villareal katika mechi ya pili ya nusu fainali ya Ligi ya Europa akiwa na jeraha la paja.

Arsenal walitolewa kwenye michuano huyo ya Ligi ya Europa baada ya kutoka suluhu, huku mchezo wa kwanza wakifungwa 2-1.







# MOURINHO kumchukua de Gea

**ROME,** Italia

KOCHA mpya wa AS Roma, Jose Mourinho anamwania golikipa wa Manchester United, David de Gea.

Baada ya kutangazwa kama kocha mkuu wa timu hiyo ya Serie A, Mourinho tayari ameanza kuweka mipango ya msimu ujao, na anatazamia kumleta De Gea kutoka Ligi Kuu England.

Kwa mjibu wa TodoFichajes, Mourinho mwenye umri wa miaka 58 anajipanga kukamilisha uhamisho wa De Gea, ambaye anaweza kuruhusiwa kuondoka msimu ujao.

De Gea amepoteza nafasi yake kama golikipa namba moja dhidi ya Dean Henderson, licha ya United kudaiwa wapo tayari kuendelea na golikipa huyo.

Ripoti zinasema kuwa dau la euro milioni 25 linaweza kutosha kabisa kumsajili nyota huyu wa zamani wa Atletico Madrid, wakati kikosi cha Ole Gunnar Solskjaer kikiwa na mpango mkubwa wa kupunguza bajeti ya malipo ya mshahara.




# Real yamweka sokoni Hazard

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid iko tayari kumuuza, Eden Hazard msimu huu wa kipindi cha majira ya joto, kwa mujibu wa Marca.

Real Madrid ilitumia pauni milioni 130 kumsajili Hazard kutoka Chelsea mnamo mwaka 2019, lakini ameshindwa kuonyesha makali yake.

Hazard, ambaye amekuwa nje kwa majeraha msimu huu, alianza katika kichapo cha 2-0 kutoka kwa Chelsea Jumatano kwenye mchezo wa nusu faianali ya pili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyo alikasirisha mashabiki wengi wa Los Blancos baada ya kamera za runinga kumnasa akicheka na kufanya mzaha na mchezaji mwenzake wa zamani wa Chelsea, Kurt Zouma dakika chache baada ya filimbi ya mwisho.

Hazard tangu wakati huo ameomba msamaha kwa mwenendo wake, lakini kwa mujibu wa Marca, uongozi wa Madrid umeamua uko tayari kusikiliza ofa kwa msimu huu wa joto.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Los Blancos hao wako tayari kumruhusu Hazard aondoke kwenye dirisha lijalo la uhamisho ikiwa watapata dau la euro milioni 50.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR AKUBALI KUITUMIKIA PSG

●●● Mshambuliaji huyo raia wa Brazil anatarajiwa kusaini mkataba mpya wa miaka...

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa PSG, Neymar yupo tayari kuongeza mkataba mpya wa kuitumkia klabu hiyo, kwa mujibu wa jarida la la L'Équipé.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Neymar yupo tayari kusaini mkataba mpya na atafanya hivyo ndani ya siku chache zijazo.

**Makubaliano hayo baina ya pande mbili yamefikiwa miezi iliyopita na imethibitishwa kuwa mchezaji huyo atasaini mkataba mpya utakaomweka klabuni hapo hadi Juni, mwaka 2026.**

Mshahara wa Neymar utakuwa euro milioni 30 kwa miaka mitano, pia atapata 'bonasi kubwa' endapo PSG itashinda Ligi ya Mabingwa Ulaya katika miaka ijayo wakati akiwa katika timu hiyo.

PSG pia wanaandaa tangazo kubwa la kusherehekea kumtambulisha mshambuliaji huyo kuendelea kusalia jijini Paris.

Hata hiyo, bado makubaliano hayajafikiwa juu ya kumbakisha Kylian Mbappe na mazungumzo yanaendelea ili aongeze mkataba wake.

PSG inatajwa pia kuwa katika mipango ya kumsajili mshambuliaji wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Salah.

Nyota huyo wa zamani wa AS Roma amekuwa katika kiwango cha juu msimu huu, akifunga mabao 29 kwenye mechi 49 alizocheza na mashindano mbalimbali.

## KWA UFUPI

**TONEY AWINDWA**

LEICESTER City na Everton ni miongoni mwa klabu zinazojiandaa na mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Brentford, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 25. (***Athletic***)

**BALE KUBAKIA SPURS**

MWENYEKITI wa klabu ya Tottenham, Daniel Levy atampa kocha ajaye wa klabu hiyo nafasi ya kumsainisha tena mshambuliaji wa Wales, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 31, kwa mkopo kutoka Real Madrid kwa msimu wa 2021-22.

**SANCHO SAFARI IMEIVA**

KLABU ya Borussia Dortmund itamwachia mchezaji wa kimataifa wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 21 kuondoka klabuni hapo kwa kitita cha pauni milioni 87.(***Mail***)

**HAALAND NJIA PANDA**

MTENDAJI Mkuu wa klabu ya Borussia Dortmund, Hans-Joachim Watzke amerejelea msimamo wa klabu kuhusu mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United, Liverpool, Manchester City, Chelsea, Barcelona na Real Madrid-hatauzwa. (***Metro***)

**NEWCASTLE, ATALANTA VITANI**

NEWCASTLE United na Atalanta zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili mlinzi wa Vitesse Arnhem, Danilho Doekhi mwenye umri wa miaka 22, ambaye pia anahusishwa na taarifa za kutolewa 'macho' na Norwich City. (***De Telegraaf***)

**LEWANDOWSKI SOKONI**

WAKALA wa Robert Lewandowski, Pini Zahavi anajiandaa kutia msukumo kwa Bayern Munich kumpa mkataba mpya mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Poland au kumuuza katika klabu ambayo itaweza kmmudu dau lake. (***Bild***)

**YOUNG KUREJEA WATFORD**

KLABU ya Watford imefanya mawasiliano na Inter Milan juu ya mlinzi wa England, Ashley Young mwenye umri wa miaka 35, kuhusu kurejea kwenye klabu hiyo, ambako alianzia kucheza. (***Watford Observer***)

**UNITED KUWEKWA SOKONI**

FAMILIA ya Glazer inaweza kushawishiwa kuiuza Manchester United, na inasemekana klabu hiyo itauzwa kwa dau la pauni bilioni nne. (Times, subscription required)

**LINGARD ATAKIWA NICE**

KLABU ya Nice ya Ufaransa, imeendelea kuonyesha nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United, Jesse Lingard baada ya kumkosa alipojiunga kwa mkopo West Ham. (***Sky Sports Italia***)

**SCHAR MAMBO SAFI**

NEWCASTLE United ina nia ya kumwongeza mkataba mchezaji wa kimataifa wa Uswisi, Fabian Schar mwenye umri wa miaka 29. (***Northern Echo***)

**SPURS YAMFUATA AARONS**

KLABU ya Tottenham Hotspur imejaribu kufanya mawasiliano kwa ajili ya mchezaji wa Norwich na mlinzi wa England anayechezea kikosi cha umri wa chini ya miaka 21, Max Aarons mwenye miaka 21. (***Football Insider***).

# MWAKINYO ATAHADHARISHWA AKIJIANDAA KUMVAA BRENDON

**Na Mwandishi Wetu**

BONDIA Mtanzania Hassan Mwakinyo, anatakiwa kuwa mwangalifu katika pambano lake la kuwania ubingwa wa Afrika (ABU) wa uzito wa Supewelter dhidi ya mpinzani wake, Brendon Denes kutoka Zimbabwe litakalofanyika Mei 28, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Next Door Arena, Masaki jijini Dar es Salaam.

Hali hiyo inatokana na rekodi za mpinzani wake ambaye mpaka sasa amepigana mapambano nane na kushinda yote huku mapambano matano akishinda kwa knockout (KO).

Rekodi zinaonyesha bondia huyo hatabiriki kwani amekuwa akishinda kwa KO katika raundi tofauti na hivyo anaweza kumpa shida Mwakinyo katika pambano lao lililoandakiwa na kampuni ya Jackson Group Sports ambapo mashabiki watalipa Sh. 50,000 kwa viti vya kawaida na Sh. 200,000 kwa viti maalum.

Tikieti hizo zinapatikana kupitia 'app' za nilipe na ontapp.

**Rekodi hizo zinaonyesha kuwa Brendon ameweza kushinda katika raundi ya sita dhidi ya bondia, Mikka Shonena katika pambano lililofanyika Desemba 12, mwaka jana kutwaa ubingwa wa Afrika wa WBF.**

Kabla ya hapo, alitwaa ubingwa wa WBO katika raundi ya 11 dhidi ya Limbani Chikapa wa Namibia, pambano likifanyika kwenye ukumbi wa Windhoek Country Club Resort, Windhoek Septemba 28, mwaka juzi. Pia aliweza kushinda katika raundi ya kwanza, nne na pili katika mapambano mengine.

Rekodi za Mwakinyo zinaonyesha mara nyingi ameshinda kati ya raundi ya kwanza na tano katika mapambano yake 12 ambayo yote ameshinda kwa KO. Pia Mwakinyo ameshinda mapambano sita kwa pointi na kupoteza mawili tangu aanze kuzichapa.

Kwa upande wake, Mwakinyo amesema kamwe hatishwi na bondia huyo zaidi ya kujiandaa vyema ili kuweza kushinda ubingwa huo. Mwakinyo alisema kwa sasa anajiandaa vyema na pambano hilo na lengo lake kuendeleza ushindi ili kutawala katika mchezo huo.

"Nipo katika mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, lakini si kigezo cha kuacha kufanya mazoezi, bado naendelea tena kwa nguvu zaidi, lengo langu ni moja tu, kuwapa raha Watanzania kwa ushindi," alisema Mwakinyo.

Bondia huyo aliweka wazi ameongeza muda wa kufanya mazoezi ili kujiimarisha na kuwa vyema kwenye nafasi ya kukabiliana vyema na mpinzani wake huku akisema pia kamwe hawezi kumdharau.

Mbali ya pambano hilo, bondia Ibrahim Class naye atazichapa na Sibusiso Zingangwe wa Afrika Kusini wakati Shaaban Jongo atachuana na Mnigeria, Olanrewaju Durodora wakati Mbulgaria Pencho Tsvetkov atazichapa na Mmalawi Limbani Lano huku nyota wa kike kutoka Bulgaria, Joana Nwametue ataonyeshana kazi na Mzimbabwe Chiedza Namakoma.




Washiriki wa kozi Iliyoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kwa ajili ya Watathimini wa Waamuzi na Utengenezaji wa Zana za kufundishia, wakiwa kwenye picha ya pamoja na wakufunzi wao. Kozi hiyo ilikuwa ya siku tano na ilifanyika kwenye ofisi za TFF zilizoko Karume Ilala jijini Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# Vita ya Pamba, Geita hapatoshi

**Na Adam Fungamwango**

VITA kubwa ya kugombea kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara ipo kwenye Kanda ya Ziwa kwa timu za Geita Gold ya Geita na Pamba ya jijini Mwanza kutokana na kuendelea kushinda mechi zao, huku zikifukuzana.

Ijumaa iliyopita, timu zote zikiwa nyumbani zilipata ushindi wa bao 1-0 na kuendelea kujiimarisha katika mbio za kupanda daraja kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara katika msimu ujao wa 2021/22.

Pamba iliichapa Kitayosce bao 1-0, huku Geita Gold ikiidungua Rhino Rangers goli 1-0 kwenye mechi za Kundi B, huku ikishuhudia Kundi A, tayari Mbeya Kwanza ikiwa imeshapanda daraja. Kwa matokeo ya timu hizo ni kwamba Geita Gold inaongoza kundi hilo ikiwa na pointi 34, huku Pamba ikishika nafasi ya pili baada ya kufikisha pointi 33, kila timu ikicheza mechi 15, zikiwa zimebakisha mechi tatu kila moja.

Moja kati ya timu hizo inatarajiwa kupanda Ligi Kuu, inakayobaki itakwenda kucheza mechi ya mtoano.

Iwapo Pamba itapanda haitokuwa mara ya kwanza kwani ni timu maarufu nchini iliyocheza Ligi Kuu Bara miaka ya 1980 na kuleta upinzani mkali, ikizalisha wachezaji wengi waliokwenda kuzichezea Simba na Yanga baadaye, ikateremka mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Itakuwa ni mara ya kwanza kwa Geita Gold kupanda na mara mbili mfululizo ilishindwa kufanya hivyo ikifungwa kwenye mechi za mchujo, msimu uliopita ikifungwa na Mbeya City.

# Vijana watakiwa kuthamini sanaa

**Na Daniel Sabuni, ARUSHA.**

VIJANA wameshauriwa kuchangamkia fursa za ajira zilizopo kwenye sanaa ili waendeleze na kumudu maisha yao ya kila siku wakati wakisubiri ajira za fani walizosomea badala ya kuzurura au kukaa vijiweni.

Ushauri huo ulitolewa na Ofisa Utamaduni wa Jiji la Arusha, Benson Maneno wakati akizindua tamthilia ya Inspekta Uchwara, yenye malengo ya kuelimisha jamii kuhusiana na ajali za barabarani na watembea kwa miguu.

Maneno altoa pongezi kwa kundi la vijana 40, linalofahamika kwa jina la "Worriors from the East" kwanza kujiajiri kupitia sanaa ya tamthilia ya maigizo na kuwashawishi Watanzania wapende bidhaa za ndani badala ya kuangalia tamthilia za nje zinazotafsiriwa kwa lugha ya kiswahili.

"Naomba vijana tuige mambo mazuri ya vijana wenzetu kama hawa, wana bendi yao na wanapoimba muziki wanalipwa, leo wameingia mkataba na Ndago Tv ili kufikisha ujumbe kwa jamii kupitia tamthilia yao inayohusu watembea kwa miguu, watapata pesa na maisha yataendelea, tusibweteke," alisema Maneno.

Alikishauri kikundi hicho kushawishi Watanzania kupitia tamthilia za vichekesho, watembelee vivutio kwenye hifadhi za Taifa ili kuimarisha sekta hiyo ambayo imeathiriwa na ugonjwa wa Corona.

Naye Kiongozi wa kundi hilo, Lwanda Magere alisema kikundi chao ambacho kilianzishwa mwaka 2003 kimeweza kukidhi mahitaji ya familia na maisha yao kwa ujumla kutokana na fedha wanazopata kwa kutumbuiza katika hafla na sherehe mbalimbali.

# Simba Queens yazidi kung'ara

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi, Simba Queens wameendelea kujiimarisha kileleni baada ya kuifunga Kigoma Sisterz mabao 4-2 katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Mo Arena jijini Dar es Salaam.

Ushindi huo umeifanya timu hiyo inayofundishwa na Kocha Mkuu, Mussa Hassan 'Mgosi' kufikisha pointi 48 baada ya kushuka dimbani katika michezo 18.

Nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo inashikiliwa na watani zao, Yanga Princess yenye pointi 44, lakini wana mechi moja mkononi huku JKT Queens ambayo pia ina nafasi ya kutwaa ubingwa inafuata ikiwa na pointi 42.

Tayari Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imeshatangaza kuishusha madaraja mawili ES Unyanyembe ya Tabora baada ya kushindwa kutokea uwanjani katika mechi dhidi ya Yanga Princess mwezi uliopita.

Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania inatarajiwa kumalizika ifikapo Mei 17, mwaka huu na bingwa mpya mwakani atashiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake.

# Michezo

Jumapili Mei 9, 2021

Nipashe




## Neymar akubali kuitumikia PSG

HABARI UK 22




Basi lililobeba wachezaji wa Yanga likiondoka kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa huku mashabiki wake wakilisindikiza baada ya uongozi kutokubali uamuzi wa kubadilisha muda wa mchezo wao dhidi ya Simba, ambao awali ulitarajiwa kufanyika kuanzia saa 11:00 jioni na kusogezwa hadi saa 1:00 usiku. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# PAMBANO LA WATANI WA JADI UTATA WATAWALA

## ●●●Ni baada ya kuahirishwa, kisa Yanga kugomea mabadiliko ya muda...

**Na Saada Akida**

PAMBANO la marudiano la Ligi Kuu Tanzania Bara lililotarajiwa kuwakutanisha watani wa jadi nchini lililokuwa linasubiriwa kwa hamu na mashabiki wa soka ndani na nje ya nchi, limeahirishwa.

Hatua hiyo ilitangazwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) baada ya kutokea sintofahamu iliyosababisha kusogezwa kwa mchezo huo kutoka muda uliopangwa saa 11:00 jioni hadi saa 1:00 usiku.

TFF, kupitia kwa msemaji wake, Clifford Mario Ndimbo, ilitoa taarifa ya kusogezwa kwa mchezo huo, huku ikidai kwamba ni maagizo kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo bila kutoa ufafanuzi.

Muda mfupi baada ya taarifa hiyo ya TFF, Yanga ilitoa taarifa ya kupinga kusogezwa mbele kwa pambano hilo kwa madai kwamba limekiuka kanuni za uendeshaji wa Ligi Kuu.

Pamoja na kupinga, timu hiyo yenye makao yake makutano ya Twiga na Jangwani, jijini Dar es Salaam, ilisisitiza kupitia taarifa yake kwa vyombo vya habari kwamba itapeleka timu muda uliokuwa umepangwa awali.

TFF ilitangaza mabadiliko hayo saa nane mchana (saa tatu kabla ya muda wa awali wa kuanza mechi), baada ya kupokea mwongozo kutoka katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Yanga ilisema imepokea kwa masikitiko taarifa hiyo ya mabadiliko ya muda wa kuanza kwa mchezo yaliyotolewa na TFF kwa madai kwamba yanakwenda kinyume cha Kanuni ya 15 (10) ya Ligi Kuu inayohusu taratibu za mchezo.

"Mabadiliko yoyote ya muda wa kuanza kwa mchezo yatajulishwa ipasavyo kwa pande zote husika za mchezo angalau saa 24 kabla ya muda wa awali," taarifa ya Yanga ilinukuu kanuni hiyo.

Iliongeza kwa kutokana na kanuni hiyo, iliweka msimamio wake kwamba itapeleka timu uwanjani muda uliokubaliwa awali na kutaka Bodi ya Ligi na TFF kuendesha ligi kwa kuzingatia na kuheshimu kanuni zilizowekwa.

Kama ilivyokuwa imeahidi, Yanga iliingia uwanjani hapo saa 10:18 jioni wakitumia geti la nyuma ya uwanja huo ambalo kawaida hutumiwa na waandishi wa habari wakiwa wanakwenda kwenye chumba maalum cha mikutano.

Baada ya basi kuwasili, walioanza kushuka ni benchi ya ufundi likiongozwa na Kocha Mkuu Nasreddine Nabi halafu wakafuatia wachezaji na kiungo, Feisal Salum 'Fei Toto' akiwa wa mwisho kuteremka katika basi hilo.

Baada ya hapo, timu iliingia uwanjani na wachezaji wake kufanya mazoezi kisha kwenda kwenye vyumba vya kupumzikia kusubiri muda wa mchezo. Baada ya muda huo kufika, timu iliingia uwanjani na kusubiri kwa muda wa dakika 30.

Kikosi cha Yanga kiliondoka uwanjani hapo saa 11:48 jioni baada ya kikao cha muda mfupi kilichoendeshwa na viongozi wa Yanga akiwamo mwenyekiti, Dk. Mshindo Msolla.

Simba nayo iliingia uwanjani majira ya saa 11: 23 kwa basi maalum la timu hiyo ikiongozwa na Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, alikiongoza kikosi chake uwanjani kwa ajili ya kufanya mazoezi mepesi ya kujiandaa na mchezo huo ambao ulitarajiwa kutoa mwelekeo katika mbio za kuwania taji la ligi hiyo.

Wakati wakiendelea na mazoezi hayo mepesi, lilitolewa tamko kwamba mechi hiyo imeahirishwa.

Hadi tunakwenda mitamboni, hakuna taarifa yoyote ya wizara, bodi ya ligi na TFF kuhusu hatima ya mchezo huo ambao unazihusu timu mbili kongwe katika soka nchini, zenye ushindani na wingi wa mashabiki.

Kwa upande wa Simba, wenyewe walisema hawakuwa na shida na kueleza ubora wa kikosi chao watacheza muda wowote watakaoambiwa na wasimamizi wa soka.

"Simba iko tayari kucheza hata usiku wa manane, kwa kuwa TFF na wizara wamesema, tuko tayari, raha ya kiporo ukile usiku kabla ya hakujakuchwa," Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara alisema.

Juma Mkamba, mwanachama wa Simba wa Tawi la Pambanano mwenye kadi namba 250 alisema hawaoni tatizo lolote kwa mabadiliko hayo kwa sababu muda wowote wanaweza kucheza na kupata matokeo mazuri.

"Kwa upande wetu hatuna presha na huo muda ukizingatia tumecheza mechi zetu jioni na hasa saa 1:00 usiku na tukapata matokeo mazuri, hao wanaolalamika ni kutokana na imani na mashaka ya timu yao," alisema Mkamba.

Wakati sintofahamu hiyo ikiendelea, lakini kikosi cha Yanga kikiwa kinaendelea na mazoezi mepesi ya kupasha mwili, baadhi ya mashabiki wa klabu hiyo walianza kuondoka uwanjani na kurejea majumbani kwao.

Uamuzi wa kuondoka ulitokana na kuwapo kwa madai kuwa uongozi wa timu yao unajiandaa kuiondoa timu hiyo uwanjani baada ya kuendelea na msimamo wa kutobariki mabadiliko ya muda wa kuanza kwa mchezo huo wa kiporo.

Simba ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na pointi 61 baada ya kucheza mechi 25 wakifuatiwa na Yanga yenye pointi 57 lakini imeshuka dimbani mara 27 huku Mwadui FC yenye pointi 19 wakiburuza mkia.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042